

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

SIRISIA CONSTITUENCY,

AT CHWELE MARKET

ON

SATURDAY, 30TH JULY 2002

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS

SIRISIA CONSTITUENCY, AT CHWELE MARKET

HELD ON SATURDAY, 30TH JULY, 2002

Present:

Com. Bishop Bernard Njoroge
Com. Paul Wambua
Com. Ibrahim Lethome Asmani

Secretariat in Attendance:

Triza Apondi - Programme Officer
James Macharia - Asst. Programme Officer
Lydia Moraa - Verbatim Reporter

Meeting was called to order at 09:40 a.m. with Com. Ibrahim Lethome in the chair.

Prayers – Fr. Francis: Kwa jina la Baba na la Mwana na Roho Mtakatifu. Ewe Mungu Baba Mwenyezi tunaomba kwamba siku ya leo hii, tunapokutana hapa kama Division ya Chwele kuchangia maoni yetu katika Katiba tunaenda kutengeneza, tunaomba utupe hekima ili tuweze kujadiliana yale ambayo yatatusu sisi kama wananchi wa Kenya kwa Kenya ambayo tunahitaji na pia Baba tunaomba hawa maCommissioners ambao wamekuja kusikiza maoni yetu uwape hekima nao pia

waweze kuweka pamoja maoni yetu ili Katiba tutakayotengeneza iwe kweli Katiba ya wananchi. Na wananchi ambao watatoa maoni yao Baba tunaomba uwatoe uoga ili waweze kutoa maoni yao bila kuwa na wasiwasi wote wakijua ya kwamba hii ni nchi yetu na hii Katiba ndio itakayotulinda kwa miaka mingi inayokuja. Tunaomba haya yote kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo Amen. Kwa jina la Baba la Mwana na la Roho Mtakatifu.

Com. Wambua: Asante sana Father kwa maombi. Sasa kwanza nitawajulisha walioko hapa. Tuko watatu maCommissioner ambao watakuwa kikao hiki hawajafika walikuwa watoke huko Bungoma. Mimi nikawa nililala karibu kwa hivyo nikafika mapema. Lakini hakuna haja ya kungojea taratibu ziko, wale ambao wananasa sauti zenu wako, kwa hivyo tunaweza kuanza halafu watakapofika tutawajulisha kwenu. Lakini wao ni Commissioner Bishop Bernard Njoroge ambaye ndiye alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa kundi hili na yule mwingine mwenzake ambaye bado wako pamoja anaitwa Commissioner Lethome Asmani. Nami naitwa Commissioner Paul Musili Wambua na watakapofika nitawajulisha. Lakini tuko na wenzetu wengine hapa ambao tumetoka na wao kule kwa Tume, ambao wanatusaidia kuhakikisha ya kwamba majina yameandikwa na ya kwamba kile mmoja wenu amenaswa sauti yake. Na hawa ni kama Triza Apondi, ambaye yuko pale ni Programme Officer kwa Commission, wa pili ni James Macharia namuona pale na yeye pia ni Asst. Programme Officer wale wanaandika maneno yote unayotaja. Na hapa tuko na Lydia Moraa, Moraa ndiye mnaona anatumia hizo tapes kunasa sauti, hakuna neno lako litakalopotea. Ukizungumza ikichukuliwa huko itaandikwa. Kama huko itapatikana itaingia kwa tape. Nasi tuko hapa kama Commissioners kusikia.

Kwa hivyo taratibu ambazo tutatumia ni kama ifuatavyo. Ukija hapa utajiandikisha huko tutatumia hiyo orodha ambayo tumepewa hapa na yule ambaye amefika kwanza ndiye tutamsikiza kwanza, first come first heard, na yule ambaye amejiandikisha kwanza ni George Sitati Wekesa, tutamuita saa hii, lakini ukija hapa unaweza kuzungumza bila maandishi. Unaweza kuwa umebeba maandishi hapa ambayo umeandika maoni yako. Ukitupatia tutayaandika huku, yatakuwa registered halafu utatuachia maandishi tutaenda kusoma. Ukija hapa usisome maandishi maanake sisi tutaenda kusoma, taja yale ya muhimu tu – highlights, ile key issues halafu yale mengine tutaenda kusoma. Tutakupatia muda wa dakika tano. Ukija kama huna maandishi tutakupa muda tu uzungumze lakini ijapokuwa hujaandika bado tutakupatia muda mchache tu utaje yale ya muhimu. Ikiwa mambo yamezungumzwa yametajwa hakuna haja ya kurudia maanake tayari tumeyapokea. Kwa hivyo usirudie maanake uchukue muda mrefu maanake tunataka tumpe kila mtu nafasi ndio atoe maoni yake.

Kwa hivyo ukishamaliza kutoa maoni yako utajiandikisha huko ndio tujue ni kina nani walizungumza hapa na waliotoa maoni. Na ikiwa ushamaliza kuzungumza sisi kama maCommissioners ikiwa kuna mtu ama mambo ambayo hatukuelewa tunaweza kukuuliza maswali ndio ufafanue. Na mwisho kabisa unaweza kuzungumza ukitumia lugha ya Kingereza ama Kiswahili, kama Kingereza na Kiswahili kinakusumbua kidogo pengine unaweza kutumia lugha ya hapa na hiyo nafikiria ni Bukusu. Halafu tuko na mtu wa kutafsiri, mkalimani ambaye atatueleza yale ambayo unasema. Lakini hakuna haja ya kusema kuwa niko hapa Chwele nitasema Kibukusu ijapokuwa naelewa Kiswahili na Kingereza, hakuna haja. Maanake unazungumza nasi kama Commissioners. Kile tunataka ni kuelewa maneno ambayo unataka kuyatoa. Usizungumze kinyumbani maanake utaharibu

wakati saa zile unazungumza na mtu mwingine anatafsiri muda unapotea. Kama unaweza kutuzungumzia kwa Kiswahili ama Kingereza itakuwa sasa tuna-save wakati. Hakuna haja ya kupoteza wakati. Hakuna haja ya kuharibu wakati mrefu eti huyu anasema na huyu anatafsiri kama unaelewa hii lugha. Lakini kama kweli kuna mwenzetu ambaye hawezi kuzungumza Kiswahili hawezi kutoa maoni kwa Kingereza basi tutampa nafasi azungumze Kinyumbani, halafu tutatafsiri.

Nafikiria tuko na mama mwingine hapo nafikiria – ni wewe, aliniambia anaitwa Christine na yeye anaongea kwa ile lugha nyingine kama kuna mwenzetu hapa haelewi lugha ya kawaida ambayo tunatumia mdomo yeye atatumia mikono kueleza yale ambayo yanaendelea. Kama mnajua kuna mtu hapa haelewi ama hawezi kufuata vile tunavyoendesha mambo hapa, basi tueze ndio tumuambie Christine atafsiri, ako pale. Kwa hivyo tutaanza na tukianza tutaimuita yule ambaye alijiandikisha kwanza hapo George Sitati Wekesa, ako wapi? Basi Wekesa utaketi pale halafu taja jina lako kwanza linaswe halafu kwa muda usiozidi dakika tano sema yale yako kwa memorandum halafu ujiandikishe hapo.

George Sitati Wekesa: Mimi kwa majina najulikana kama George Sitati Wekesa. I propose for a Federal form of governance which should comprise of a Central Government, the Federal Government and various smaller Governments established at provincial level. All provinces put together form a federation. Each province to have its Governor, Legislature and Judiciary. There should be two sets of laws applicable – the federal law made by the Central Legislature and Provincial Law made by the Provincial Legislature and applicable only within its province. A citizen can decide to live in any of the provinces regardless of his or her place of birth provided that he or she abides by the laws of that province. The Federal Government to be in charge of the whole country and to be in control of the following:-

- Constitutional Affairs
- Financial Affairs – e.g. Federal taxation and monetary policy
- Foreign affairs and national security and
- Immigration and citizenship.

And Provincial Government to be in charge although not exclusive of certain affairs namely local health, local infrastructure, local education and provision of sanitary services e.g. water and sewerage disposal. Law state Government may make a law that contradicts the Constitutional of the federal law. Federal Government will ensure that our country is effectively managed, this will necessitate devolution of power from the centre to the provinces. Some leaders in Kenya have been talking about majimbo system without understanding the fundamentals of federal Government. Such leaders have argued that federal system would mean people going to areas where they were born or tribes to which they belong. That is a colonial majimbo system which was based on ethnic bigotry and which had very little federal content, in fact some a system can only lead to bacanisation of a country if not outright cessation of some parts.

Another point which I would like to talk about concerns Presidency. A person shall not be eligible for election or tenure as

President if he or she intends to contest as a Member of Parliament and therefore I propose that the President shall not represent any constituency as its Member of Parliament and this should also apply to the Vice President. This will make it easy for them to concentrate on national issues, as they are symbols of national unity.

Another point, about appointment of Ministers, I propose that the Ministers and deputy Ministers to be appointed from among citizens qualified for elections as Members of Parliament. Members of Parliament appointed as Ministers or Deputy Ministers should cease to hold their seat in Parliament upon such appointments.

Another issue which I would like to talk about concerns Constitutional Amendments. I propose that the Constitution shall only be amended if a bill providing for the amendment of any provision is supported on a second and third reading by at least 75% of the members of the National Assembly excluding the ex-officio members and a National Referendum has been conducted in accordance with the Constitution approving the proposed amendment and the proposed amendment is subsequently supported by at least two-thirds of the Members of Parliament.

Another issue that I would like to talk about is international treaties. Parliament shall have the exclusive power to ratify all international treaties, agreements or conventions with a two-thirds majority. Any international treaty so ratified shall have the force of law in Kenya.

I would also like to talk about Affirmative Action. I propose for Affirmative Action to ensure the full development and advancement of disadvantaged groups of society for the purpose of guaranteeing them equality.

And lastly I would also like to talk about Commission on gender equity. I propose for a Commission on Gender Equity which shall promote gender equality and to advise and to make recommendations to Parliament or any other body with regard to any law or proposed legislation which affects gender equality and the status of women. Thank you.

Com. Wambua: Bwana Sitati nitakuuliza swali. Let me ask you a question. When you propose that Parliament should approve international treaties by two-thirds, are you proposing that the approval should be sought and obtained before we sign the treaties or is it after the treaties have been signed, then they are brought to Parliament for approval? Which proposal do you have, I didn't get that very clear?

George Sitati Wekesa: Okay. International treaties. Parliament should have the exclusive power to ratify all international treaties and agreements and conventions with a two-third majority before.

Com. Wambua: Before it is ratified?

George Sitati Wekesa: Before it is ratified.

Com. Wambua: Okay, thank you very much. Asante sana jiandikishe hapo Bwana Wekesa.

George Sitati Wekesa: Thank you.

Com. Wambua: Thank you for your views, which are very good, which we will take into account. Wilfred Kisuya from the Association of Physically Handicapped, I believe you have a lot to say about the disabled. Please mention your name, the association you represent. Give us your proposals.

Wilfred Kisuya: Thank you very much. My names are Wilfred Wabwoba Kisuya, the Secretary-General of Association of Physically Handi-capped, Kenya. I propose the following to the needs and basic needs of the disabled.

- (1) Kenya to have disability revolving fund to cater for the needs of the disabled.
- (2) A disability service commission be formed to implement development progress of the disabled e.g. training, education, social, medical and economic participation of the disabled.
- (3) All disability appliances be given free regardless of gender and disability.
- (4) The National fund for the disabled of Kenya be manned by the disabled.
- (5) The disabled be represented in Parliament through fair and free elections.
- (6) All basic needs of the disabled be given as where and when need arises.
- (7) During all the fiscal year budget of the Kenya Government funds be allocated aside to meet the basic needs of the disabled to cater for their social and economic participation.
- (8) Special schools be available from district level and above for the purpose of empowering the disabled to participate equally.
- (9) Among the needs of the disabled, all disability organizations worldwide including Kenya among them, be given chances for participation through Parliament or any approved organization to meet and cater for their needs. Thank you.

Com. Wambua: I want to ask you a question Bwana Wilfred Kisuya. One of the issues we have been given views on is the question of integrating the system of education to ensure that we do not have special schools for the handicapped. The visually handicapped, mentally handicapped that they should be integrated into the normal schools and that will help them learn to live that those who are not disabled should know how to live with the disabled persons. What is your view on that, should we integrate the system or should be set aside? I notice that you talk of special schools, but what is your view on the integration, should we be integrated or should we not be integrated?

Wilfred Kisuya: My view about the integration should be, like this way I am talking may be you might have an integration system but its not on district level. So I think you must have that indication. We must have the same.

Com. Paul Wambua: Inaudible.

Wilfred Kisuya: Okay, thank you. We have two types of disabilities. We have mental, physical, visual and what have you. So at least we just have different schools for the same.

Com. Wambua: Thank you very much. Please register yourself there. Asante sana kwa maoni yako. Moses Simiyu Lusano. Moses taja jina na utupatie maoni yako tafadhali.

Moses Simiyu Lusano: My name is Moses Simiyu Lusano from Chengeni I represent Misambwa Group. I contribution to this:-

- (1) Land problems: Land was surveyed some years back but today the fee or tax is very high. We need land to be resurveyed after five years. Most of the poor people are unable and so it has become very difficult for anybody to own land because of that high taxation.
- (2) The President's decree to be taken to Parliament. I say this because sometimes there things which are enforced and then people find it very difficult.
- (3) During the World Cup, I saw policemen arresting people who were watching TV, watching the matches on TV. I ask the Government to see to it that such unnecessary harassment is removed.
- (4) I come to police cells and prisons. When you go to police cells and prisons the prisoners are no better than slaves, they are enslaved. So let a good Government check on this system. People are dying there like flies and when someone takes you there, it means he has taken you to the grave. To come back out of there it will just be God's wish.

- (5) I come to customary law courts: Kenya belong or has got very many ethnics groups and they have got different customs. So I think or I suppose the Government should establish a customary court to be dealing with this.
- (6) I come to freedom of conscience. There were people who fought for our Uhuru or freedom. These were Misambwa Uhuru fighters. Really these people are not considered because they have not been rewarded and even they are restricted not to continue with their sect or worshipping. So I urge the good Government to consider these people are then reward them something.
- (7) I come to our capital city Nairobi – it is congested and I propose that let the Government establish a capital city elsewhere and Nairobi remain a trading centre.
- (8) I come to Judiciary: Poor people are not well represented in courts because they don't have lawyers to represent them, so I propose the Government to hire lawyers for such people who are unable to represent themselves.
- (9) I will talk about Mount Elgon forest which is dying. When you look at our rivers now we have less water because that catchment area has been destroyed completely. May the good Government help us to replant the trees once more.
- (10) I come to farmers who grow coffee. The first area to grow coffee in Bungoma District or Western was Chwele. Upto now coffee has made the farmers in this area to suffer a lot and even our capable children who could pursue higher education are unable because the parents are unable to raise any amount. So I propose let the good Government build coffee millers in Western or in these areas, so that we cannot take our coffee to Nairobi and then we don't know what goes on there.
- (11) In addition to that, in this area guavas grow widely. So I propose the Government to make some light industries in this area, so that this will help to employ our people or school leavers.

Thank you, that is the much I can contribute.

Com. Wambua: Thank you very much. I think I will have to announce the arrival of two of my colleagues, kama nilipotaja tulikuwa na macommissioner wengine wawili ambao walikuwa njiani kufika hapa, wamefika. Tuko na mwenyekiti wa kikundi hiki ambaye ako karibu nami hapa Bishop Bernard Njoroge, Commissioner, tuko na Commissioner mwingine mwenzangu hapa Commissioner Ibrahim Lethome Asmani. Sasa hawa ndio tutaendesha nao kipindi ama kikao hiki.

Nafikiria mama D.O. utatukaribisha hapa maanake ni kwako tulipoanza hukuweco, tulianza tukaona hatutaweka watu tu, kwa

hivyo utaongea machache. DO wa area hii ako hapa nasi Caroline Onjoka. Kwa hivyo mama utataja machache utukaribishe, halafu tutaendelea. Kikao sasa kitaendeshwa na Commissioner Asmani Lethome ambaye nitampatia sasa nafasi aendeshe baada ya DO kuongea.

Caroline Onjoka – DO: Asante sana Commissioners wetu, viongozi wa sehemu hii ambao wamefika wakati huu, nataka kuwakaribisha kirasmi katika tarafa ya Chwele ili mtoe maoni yenu kama wakaaji wa sehemu hii. Kwa hivyo mmekaribisha wanaCommissioners wetu, hawa wamekuja nafikiri wengine bado wanakuja. Lakini ningewasihi kama inawezekana tutoe maoni kwa wingi kabisa. Kila mtu aweze kupata nafasi, ukijaliwa kupewa nafasi ujaribu kuharakisha ili wale wenzako wapate nafasi. Na pia ukimaliza kama unarudi nyumbani waambie wale wengine wanakuja. Lakini naona wakina mama ndio hawajakuja. Nafikiri wako njiani wasipike chai na ugali mpaka wachelewe. Kwa hivyo wazee mkienda mwapatie nafasi, huu ni wakati mzuri sana kama sisi Wakenya wa sehemu hii kupewa nafasi ya kutoa maoni kwa kuandikisha Katiba yetu. Kwa hivyo Commissioners wetu tafadhali mjisikie uhuru, muwe nyumbani muendeleo kukaa na hawa watu wetu wakitoa maoni yao. Asanteni.

Com. Wambua: Nafikiria tutataja District Co-ordinator wa Bungoma ambaye ako hapa na ninafikiria mnamjua. Mr. Walinywa ambaye ndiye anahusika kupanga mipango ya sehemu ya Bungoma. Kwa hivyo sasa Commissioner Lethome chukua usukani uendeshe kipindi.

Com. Lethome: Asante sana Commissioner Wambua. Watu wa Chwele Mlembe. Sawa, sasa tuendeleo, hiyo ndiyo Kibukusu ile ninajua, sijui ingine. Haya Justus Wabwire Nabiswa kutoka Usambwa.

Justus Wabwile Nabiswa: Nitaongea vile mwenzangu ametoka alikuwa kijana na msiseme ya kwamba narudia maneno yenyewe. Mtaniruhusu kidogo niongeze maneno, sitarudia yale ambayo ameyasema. Vile wale mashujaa waliopigania nchi yetu, nitaanza kwanza mnamo 1895 watu hawa walipinga Wazungu kuingia katika nchi yetu. Mwaka huo watu wale waliouawa katika mji au Tuhara Lumboka, na mwaka huo huo mwenyewe Webuye. Halafu wakafuatia 1908 watu wengine..

Com. Lethome: Hiyo maneno umetuambia ni muhimu sana na ni nzuri. Lakini sasa hiyo ni historia. Pendekeza.

Justus Wabwile Nabiswa: Ningetaka Katiba iliyoko kuhusu watu wale ambao waliuawa Katiba ambayo tunaiandika iwashtaki wale waliowauwa watu wetu kwa sababu waliuawa kwa ajili ya nchi yao.

Jambo la pili: Watu wale wa kikundi cha Msambwa waruhusiwe kujenga mashule, waelimishe watoto wetu, wajengewe clinic, watibu watu wetu na kazi zingine. Ningependa wafanyiwe hivyo. Na bila kupoteza wakati..

Com. Lethome: Kikundi cha Msambwa ni kikundi cha kisiasa au?

Justus Wabwile Nabiswa: Cha kidini.

Com. Lethome: Cha kidini. Kwa hivyo wapewe ...

Justus Wabwile Nabiswa: Waruhusiwe wapewe uhuru wa kuabudu, uhuru wa kuomba na uhuru wa kupata elimu kwa watoto wao. Na bila kuendelea na jambo hilo, nitaguza neno lingine. Kuhusu usalama ambapo nimesoma mahali fulani, nafikiri usalama wa raia katika nchi ya Kenya haulindwi ipasavyo katika Katiba iliyoko. Na ninataka hivi watu wengi wanauawa katika barabara, jambo la kwanza ni magari kuendeshwa mwendo wa kasi. Jambo la pili, gari kubeba watu kupita kiasi. Watu hutembea kama wamesimama wananinginia milangoni, gari mizigo nyuma mbele limebeba. Na ninaonelea ya kwamba gari lisiruhusiwe kubeba watu kama watu wamesimama. Gari liko na viti Katiba iliyoko sasa iandikwe kulinda uhai wa mtu, mtu atembe katika gari kama amekaa. Kwa sababu gari limejengwa lina viti vya kutosha, wakati wa mkoloni hatukuruhusiwa watu kutembea kama wamesimama.

Com. Lethome: Lingine Mzee.

Justus Wabwile Nabiswa: Jambo la tatu, kuhusu tu usalama. Kuna vitu kama wanyama, ng'ombe, ng'ombe akitembea barabarani anapigwa akauawa. Na hapo eti mwenye ng'ombe unashtakiwa ya kwamba wewe ulipe. Na ng'ombe hana fahamu, ng'ombe hajui kitu gani kinachokuja kutendeka.

Com. Lethome: Sasa hapo unapendekeza nini, ng'ombe akigongwa barabarani nani alipe?

Justus Wabwile Nabiswa: Aliyepiga alipe. Sio mimi kulipa. Pengine ng'ombe alikuwa tu anaruka barabara na muendeshaji gari akampiga na si wewe ukija na gari unaona yule ni ng'ombe, wewe unastahili kuhepa kupiga huyo ng'ombe. Kwa hivyo anayeu huyo ng'ombe alipe.

Com. Lethome: Na mwenye ng'ombe naye afanye nini? Huna jukumu la kuangalia ng'ombe wake asiende barabarani kwa sababu hana akili ng'ombe.

Justus Wabwile Nabiswa: Ng'ombe akiwa amepigwa hana uwezo, hana akili pengine alikuwa tu ng'ombe huyo peke yake anaenda kutafuta maji halafu ipigwe. Hapo mwenye ng'ombe hastahili kulipa kwa sababu ng'ombe haina elimu. Haya kuongeza tena mtu akiwa anatembea barabara unakuta watu wengine anauawa kando ya barabara na hapo halipwi. Kwangu naonelea ya kwamba mtu akigongwa na gari na alikuwa mkono wake, yeye aliyemuua anastahili kulipa. Hapo mimi napigania uhuru wa mtu au uhuru wa raia ya kwamba mtu yule alipwe asiwachwe bure.

Namalizia neno lingine kuhusu ardhi: Kuna kifungu mahali kinasema mimi namiliki shamba langu na nitasema tu msemu wa kifupi. Ikiwa mimi namiliki shamba langu, nikishaaga dunia naona ya kwamba eti mtu ambaye atarithi shamba hili ikiwa mke wangu atawashtaki kortini kwamba ndio wapewe huo urithi. Kwa nini washtaki, mimi singependa washtaki kwa sababu shamba hilo limejulikana, mahali ambapo nimekaa kuna serikali ya mitaa, kuna watu wa jamii wanaelewa mimi ni mwenye shamba, kwa hivyo watu wangu warithi bila neno lolote. Nafikiri kama muda ungeniruhusu ningendelea kidogo.

Kuna jambo lingine ambalo nitaliguza kuhusu sisi katika mila ya Wabukusu, kuhusu mtoto msichana. Mtoto msichana akiolewa kuna mwiko wetu au kuna kitamaduni chetu akishakwenda kwa bwana atachinjiwa mbuzi. Mbuzi huyu inamaanisha ya kwamba yeye ameolewa ni mke wa mtu yule. Sasa yule msichana akitoroshwa na mtu mwingine, kulingana na hiyo mila mtu ambaye amemtorosha atashtakiwa. Na yule msichana anastahili kukaa na bwana yake bila kuvunja ndoa. Naongea pale kwa sababu nimesikia mahali pengine ya kwamba wasichana wanataka ardhi. Akishafanyiwa hivyo yeye amepata bwana, ardhi atapata kulingana na bwana wake ambaye ameoleka huko. Asanteni.

Com. Lethome: Na yule ambaye hajaolewa msichana ama hataolewa, apewe ama aje?

Justus Wabwile Nabiswa: Kama hajaolewa, ataolewa. *Laughter.*

Com. Lethome: Asante sana. Shadrack Watima?

Shadrack Watima: Kwa majina naitwa Shadrack Watima nitazungumza kwa lugha ya Kibukusu.

Interceptions: *How do you want me to translate – summarise or?*

Com. Lethome: Summarise. Recommendations.

Shadrack Watima: *Khusakho khwikhuwa lilala.*

Translator: I want to touch one point.

Shadrack Watima: *Lubeka lwa baana besikhasi.*

Translator: About female people.

Shadrack Watima: *Khuli ne abaana befwe ngefwe babukusu.*

Translator: We have our daughters.

Shadrack Watima: *Olomaramo mima khulomalomakho.*

Translator: As it has been talked about.

Shadrack Watima: *Efwe omwana atsitsanga khu musacha mala khwana obukhwe.*

Translator: The daughter marries and we get dowry.

Shadrack Watima: *Sisiaba mukhasi uwo.*

Translator: Then she shall belong to where she has married.

Shadrack Watima: *Maala wakhwa omwana womundu aba mukhasi unono sakhayere khukenda kenda busa ta.*

Translator: Once married so she is then a wife in that home and should not loiter around or walk carelessly.

Shadrack Watima: *Nono luno ndalolanga babana balalobanga basecha ne bakenda busa.*

Translator: Today I see girls refusing their husbands and loitering about.

Shadrack Watima: *Khwenya khwisie khumwima khufwe nga abakuka babechanga.*

Translator: They used to pay dowry of eight cows.

Shadrack Watima: *Bakhwetsanga bakukhu tsikhafwa tsitaru.*

Translator: And then the marriage is confirmed by killing an animal.

Shadrack Watima: *Maala bakisa.*

Translator: Then she is complete wife of that person.

Shadrack Watima: *Aba omukhasi wa omundu.*

Translator: And when she is a wife of somebody, even when she is dead she can't be buried back in her original home.

Shadrack Watima: *Nabe omukhasi wa omundu nafwe sakabalonga wabwe ta.*

Translator: So today among the Bukusu.

Shadrack Watima: *Nono ndola andi wabukusu*

Translator: We want to reduce the dowry that has been 13 cows.

Translator: We want to reduce those 13 cows because now there are no cows.

Com. Lethome: 13 to how many?

Translator: *Wenya bakobasia tsikhafa tsinga*

Shadrack Watima: *Ndola ndi khukobola mukhafa tsama khuba sita*

Com. Lethome: Unajua, hebu sikizeni ngoja kidogo sasa tunavunja sheria, hata mchezo wa mpira uko na referee na uko na sheria zake. Sasa sheria yetu hapa nafikiri mliambiwa na Commissioner. Wakati mtu anazungumza hapa tunampatia nafasi atoe maoni yake. Wewe huko kama yale mtu anazungumza inakuuma wewe nyamaza tu, utapata nafasi yako utakuja kuzungumza. Kwa hivyo tafadhalini nyinyi mkae kimya huko, no comments, wacha azungumze akimaliza utakuja utasema yako. Sasa nitatoa "red card".

Shadrack Watima: *Tsikhafu tsibe asi wa tisa sita.*

Translator: Dowry should be between 6 to 9 cows.

Shadrack Watima: *Sikira mbolere endio.*

Translator: Why I propose so.

Shadrack Watima: *Tsikhafa musiba tsewema khulabetsanga abaana befwe kamakobi maana ofwa busa mala nibakhakhuwakho esindu ta.*

Translator: Otherwise we are demanding too much and people are not able to pay 13 cows and then because we are demanding too much, we end up getting nothing.

Com. Lethome: Okay, that point is made. Something else – tumesikia dowry – ng’ombe hizo umesema.

Shadrack Watima: *Elindi ndikho busakho khulubeka lwe abaana be kamaloba murisi.*

Translator: I want to talk about land inheritance.

Shadrack Watima: *Khuli nende etabu yimunyanga kamaloba nofire kamaloba.*

Translator: Today there are a lot of problems for people.

Shadrack Watima: *Tsikhurisia khumaloba komundu ofire khulanyalonga tsitaaba tsigarama tsingali.*

Translator: There is too much taxation and the process is slower.

Shadrack Watima: *Lolondi barusie kamaloba kaba mukhulo.*

Translator: Land should be removed from courts or whatever to clans.

Shadrack Watima: *Ekabere mukhole sikira nie ene bunyali.*

Translator: The clan has authority.

Shadrack Watima: *Abandu nibo omundu yafira kalekha bali mukholo.*

Translator: The people left behind by the dead belong to a clan.

Shadrack Watima: *Nono ndola tsigarama tsirabetsangakho notsa sa koti bakhunyanyasia afadhali khuli nene emea kamaloba.*

Translator: It is cheaper for the clan to handle the land succession than the courts.

Com. Lethome: Okay that point has been made. Something else.

Translator: *Esindu sindi.*

Shadrack Watima: *Esindu sindi ndakusiakho Mulomilomi wama khulomaloma khubarabara.*

Translator: He is going to talk about transport or road travelling.

Com. Lethome: Tell him not to recommend not to tell us the problem.

Shadrack Watima: *Khubarabara ngekhefu – malikha nikhalisia sikira rero sibarakho siokasi ekhafwa ebe khano ta nalekha busa neno ekhafwa enyala omwana atima nekhafwa ebira ne emotoka yimba maani yimba ne wekhafu ota khurunga okusie tsindukusi aba serikali khuyitasi.*

Translator: It is unfair for anyone who has his cow knocked by a vehicle pay for the damage on the vehicle and yet this is a cow that belongs to someone and has been knocked by a vehicle. It is better if the owner of the vehicle pays.

Shadrack Watima: *Ese ndolandindi ekhafu itsungwe no mundu ni imala paka wakhasia mundu ne tsimuni oba obututukhi emutoka yakhulekho accident niye mala emitoka ----amalesi akhaire wemutoka yarunge ekhafwa*

Translator: It is the person who has knocked the animal that should pay not the owner of the animal.

Com. Lethome: That point has been made. Now can he finish?

Shadrack Watima: *Ese kakasi nakamandio.*

Translator: I have ended there.

Com. Lethome: Thank you. Ngoja kuna swali Mzee.

Com. Wambua: I just wanted to confirm, I listened very carefully is he suggesting that under Bukusu customary law there was no divorce, once a woman got married she remained married until death, that is what I want to clarify.

Translator: --- *omukhasi uno karula balekhana nemusicha nomwe ta.*

Shadrack Watima: *Balekhananga nebasiri ngaluno.*

Translator: The rate at which they were divorcing is not like now but there was divorce.

Com. Wambua: But there was divorce.

Com. Lethome: Chriskellas Bellas Mutacho.

Chriskellas Bellas Mutacho: My names are Chriskellas Mutacho Wabomba. I would like to propose on two issues (1) On education; (2) On healthcare.

Education: My first proposal is that the courts and realistic governance to provide free education to all Kenyans. Now, in our country we realize that only those ones who are economically well off can educate their children.

This situation has caused so many street children of which it's causing insecurity in our country.

On the second issue, I would like that likewise the good Government to provide free healthcare to all Kenyans, because now most Kenyans who cannot afford the medical fee they are dying innocently.

On another issue which is not written in my memorandum, is that we realize that in our country Kenya we have got so many people who are learned but they have no employment. So we would like that in our country Kenya, the Government to provide at least certain amount as a way of appreciation for those ones who have learnt and are not employed anywhere. That is to get a salary despite the fact that they are not working.

Second, I would like maybe to verify on the issue of land at least the Government to simplify the procedure. That is from the High Court Nairobi, to district land board to tribunal courts and even at the divisional courts. Those are my views, issues that I would like maybe the Government to look into.

Com. Lethome: Thank you very much. Hand over your memorandum. Gerishon Walubengo – Bukusu Elder.

Gerishon Walubengo: I am Gerishon Walubengo working with Bukusu elders in Chwele division. I will give some highlights because I have a memo here, I will only give a few highlights from the memo. Now I think the long awaited Constitution should be a basis of a stable Government. That is a stable Government here means when there is some misconduct caused in the country, the Government should be held responsible because we have been having some tribal differences here and there and nobody came out strongly to point an accusing finger at the person who caused this misunderstanding between the Kenyan's

rights.

The stable Government again should be in the sense that it is an umbrella for every Kenyan be it poor, rich or tycoons for that matter. They should be equal in all aspects before the Kenya Constitution. Now, we have been having cries here and there over the economic recession in the country and this economic recession has occurred but we don't know what was the main cause of it. But personally I feel it is because people who have been put in charge of this have not been put there on merit. Therefore, if someone has been given an office and he messes up with it and fails the economy, I think the Government should be held responsible to say why such a person was given a big office and was not fitting in it.

Another one has been one way of rushing the Kenyans to stages that they have not matured to it – that is liberalization. Liberalization has caused a lot of redundancy in Kenya. Very many local industries have collapsed because of unchecked liberalization. I think if the Government wants to revive the economy they should work on how liberalization can be implemented because the liberalization we have is just open and anybody with poor goods or good quality goods comes in and sells the way he wants and liberalization the first time intention was it will create competition among the manufacturers. But that is not what is happening. Instead of our manufacturers competing they are now collapsing.

Now, I again say about the economy. Economic planners in this country have not been given enough time to go round and work with the wananchi, so that they identify some areas that can be utilized to produce proper economy. For example, we are importing hydro-electricity from our neighbouring countries but when you look at some areas in this country like Bungoma, you find that we have rivers with waterfalls. If these waterfalls are harnessed, I think Western Kenya would enjoy the hydro-electricity from the rivers around here. For example, we have Kuywa Waterfalls. It's here, its a good one. Kuywa is a permanent river throughout the year. We have another one on Nzoia.

Com. Lethome: Enough, examples are many – just one now.

Gerishon Walubengo: Another example is Nabuyole on River Nzoia.

Com. Lethome: Recommendation.

Gerishon Walubengo: Recommendation is we want the Government to harness these rivers so that hydro-electricity is produced locally here. Now we have another industry in this district of ours that is Panpaper. Panpaper they took away land from the locals and the locals are not benefiting anything from this paper mills.

Com. Lethome: What do you recommend?

Gerishon Walubengo: I recommend that they start subsidiary industries like producing matches, like producing cardboards. Because this factory only produced semi-finished products and these semi-finished products are taken to other areas and you know when they are taken to other areas, those areas that are receiving the semi-finished products are getting employment and the owners around here who gave them free land are not benefiting at all.

Another one, I would like to suggest that we have a constitutional court. The constitutional court is very very necessary because as far as I am concerned, it is very much unnecessary for the Government to have set out this Commission to go round taking the views because when you look at the current Constitution many of the things people are talking about are there. But the mistake has been the Government didn't provide a better way of making sure the wananchi have access to this current. That is one.

Two: There is no any office in this country which can watch the implementation of the current Constitution and I fear if we do not have Constitutional courts the same thing is likely to happen. We shall make this Constitution and we give it very good names or very good adjectives but if there is nobody to monitor the implementation we shall be just ground with the same zero work. Therefore, I feel Constitutional court is very very important to monitor or to be given the power to monitor the implementation of the Constitution.

Another thing is about the President: In my memorandum together with my colleagues we passed that the President should be given a term of two terms five years each. And after the two terms have ended this President cannot be allowed to contest for President, but can only be allowed to become an MP if he so wishes. I think with those highlights I will say thank you.

Com. Lethome: Thank you, hand over your memorandum please. Patrick Wanyonyi. Halafu kama kuna mama yeyote baada ya Wanyonyi, mama yeyote ambaye amejiandikisha aje hapa. We want to balance. Haya Patrick.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Kwa majina naitwa Patrick Wanyonyi Sikuchi. Na nimeshukuru sana kuja kwenu hapa hasa mimi nashukuru serikali kwa kuwatuma nyinyi hapa kwa sababu.

Com. Lethome: Pendekeza sasa.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Mapendekezo yangu ndiyo haya. Sisi hatuko uhuru, hatuko uhuru hata kidogo. Kwa sababu ni kwamba mimi sina kazi na nina mke na nimezaa watoto, na wanaenda shule. Kwa vile wanasoma sina namna na baba yangu alinipa shamba eka moja tu na nina watoto saba, pamoja na wengine.

Com. Lethome: Pendekeza sasa.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Mapendekezo yangu ni kwamba tafadhali ikiwa serikali inahudumia tuwe huru, wasiwache hawa watoto ambao sisi tunazaa anakuja kushika mimi kama baba yake na ananisukuma mbele kwa ajili ya busaa peke yake.

Com. Lethome: Sasa unataka Katiba ifanye nini kuhusu hii?

Patrick Wanyonyi Sikochi: Katiba ifanye hivi, kimila yetu mbeleni ilikuwa ya kwamba ikiwa mimi nimepanda njugu au mtama au wimbi, tulikuwa mbeleni tukifanya ya kwamba unaweza kutengeneza pombe yetu ya kimila na watu wakaja wakapalilia shamba na wakishapalilia shamba baadaye wanaweka mtungi wanakunywa hiyo pombe kwa ajili ni malipo yao.

Com. Lethome: Pendekeza sasa.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Napendekeza ya kwamba, tuwe huru lakini

Com. Lethome: Kunywa busaa.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Hapana. Sisemi hivyo. Tuwe huru kwa njia hii, ikiwa kweli pengine huenda ikawa watu wamekuja wamenisaidia kazi na pengine nimetengeneza kidogo watu wanakunya tusikimbizwe.

Com. Lethome: Yaani unataka serikali iwawachie huru busaa.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Kabisa. Ndio hiyo, hiyo ndio lengo langu.

Com. Lethome: Wacheni niwaambie kitu kimoja Wakenya. Msione DO hapa mkafikiria kuna jambo fulani ambalo ukizungumza utachukuliwa hatua, hata kama PC yuko hapa, hata President umepewa uhuru na sheria useme vile unavyotaka. Kwa hivyo usianze kupitia pitia kando hivi kama unasema tunataka busaa iwe halali, sema wazi wazi. Hata DO anajua watu wako na uhuru wa kusema vile wanataka. Amekuja hapa kutoa maoni yake kama Mkenya. Kwa hivyo usiwe na wasi wasi.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Mimi nasema tafadhali ikiwe tunakunywa busaa wasitukimbize, kwa sababu tutakuwa tumetoka kwa shamba letu kufanya kazi.

Interceptions: Limeingia hilo.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Bwana Commissioner, vile umetembea, vile umekuja hapa hata vile DO mwenyewe anaona na macho yake. Hapa kweli tuna mahindi au hakuna?

Com. Lethome: Iko mahindi.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Na walevi wanaweza lima?

Com. Lethome: Hebu niambie sasa.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Si tuna kahawa hapa tunapeleka mitambo, mlevi anaweza vuna kahawa? Anaweza lima?

Com. Lethome: Hawezi.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Hawezi, kwa hivyo tuwe huru sisi hatuna uhuru wowote. Tunanyanyaswa kabisa.

Com. Lethome: Uhuru ni kunywa busaa peke yake?

Patrick Wanyonyi Sikochi: Sio kunywa busaa. Jambo la pili, watoto shuleni kweli tuna hatari kabisa. Mara serikali inasema elimu ni ya bure.

Com. Lethome: Wewe unapenda nini?

Patrick Wanyonyi Sikochi: Mimi napenda elimu ya zamani 7-4-2-3. Thank you for your correction. Hiyo elimu irudi, kwa maana mimi nakumbuka mwaka wa hamsini na nane.

Com. Lethome: Wacha historia pendekeza, tunarudi kwa ile ya zamani.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Jambo la tatu, wasichana vile mzee Shadrack alikuwa hapa unaweza kuoia mke ukatoa mahari na ukafanya tohara. Tohara ndio alikuwa anasema (Kibukusu) that tunaita confirmation kama ring, kama kikanisa. Lakini wazazi wale wanaambia wasichana wao wanarudi wanakaa kwao na wewe ulilipa mali. Sasa anachunga bibi na mali yako. Hiyo ni mbaya.

Com. Lethome: Sasa unapendekeza nini?

Patrick Wanyonyi Sikochi: Napendekeza msichana akioleka akae na bwana yake.

Com. Lethome: Mpaka siku ya kufa.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Ndio hiyo tu kwa sababu mlikubaliana mnaenda kuishi na yeye mpaka kifo.

Com. Lethome: Hiyo imeingia, ingine.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Jambo lingine, kuhusu kimila yetu ya Bukusu. Hasa mwezi wa nane ndio huu. Kusema ukweli utaona hawa vijana wanakuja wanafukuza sisi kwa nyungu yetu.

Com. Lethome: Sasa unapendekeza nini?

Patrick Wanyonyi Sikochi: Napendekeza watupe uhuru mila ibaki mila.

Com. Bishop Njoroge: Vijana gani wanakuja?

Patrick Wanyonyi Sikochi: Wenye kuja hawa.

Com. Lethome: Sasa Mzee nilikwambia usiogope kusema kama ni hawa vijana wametahiriwa. Sema kama ni polisi, sema ni polisi.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Ni polisi. Sisi hatuko huru Kenya, hatuko huru. Hata niliona DO mwingine anatembia anatafuta chang'aa, na kumbe anapeleleza manyumba.

Com. Lethome: Sasa pia si inazuia msijiumize na hiyo kitu.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Hiyo ni kweli, chang'aa ni sawa. Mimi nakubali. Lakini busaa watuachie watupe uhuru, hiyo ni chakula, ni ugali. Hiyo ni ugali, lakini chang'aa inakuua. Sisemi hivi na mbadilishe msemi walisema tumekataa pombe, vile nakumbuka IPPG vile ilikuwako tulipitisha na baadaye wakasema Bungoma walikataa pombe, ndio wakafunga vilabu '78. Hiyo hatutaki.

Com. Lethome: Hiyo hatubadilishi ina-record. Sauti yako itafika Nairobi. Bungoma wanataka pombe.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Hiyo hatutaki kama ya '78 hiyo hatutaki. Iwe tu mtupe uhuru tukule chakula yetu lakini chang'aa mimi nakataa.

Com. Lethome: Maliza ya mwisho.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Kumaliza yangu nasema ya kwamba hilo sitasema wacha likae. Tuna njia ingine, tuko kwa siasa inakuja na tuna mapendeleo na hatutaki mapendeleo, lengo langu ni hili: ikiwa tunaenda kupiga kura mwaka huu, kama ni polling station tuhesabu kura hapo hapo. Na report iende headquarters Nairobi kwa Electoral Commission, badala ya kuenda Sirisia na masanduku ingine inatoka Toloso sijui wapi nakujia kando. La, tunataka humanitarian right. Sasa kura tuhesabie penye tunapigia, kila mama kama amekuja ametunga mlolongo anajua tumempitisha huyu ikiwa mgongo au mlolongo.

Com. Lethome: Hiyo tumemaliza. Sasa kura inahesabiwa mahali pa kupigia kura.

Patrick Wanyonyi Sikochi: Hiyo tu. Yangu imekwisha.

Com. Lethome: Haya, orio.

Patrick Wanyonyi Sikochi: *Orio mno Msakhulu.*

Com. Lethome: Haya mama *inja ano mama*. Wanaandika jina lako kuweka record ya historia. Sema jina lako mama na uendelee.

Rose Wanyonyi: Asante. Kwa majina naitwa Rose Wanyonyi.

Com. Lethome: Hebu tunyamazeni tumsikize mama.

Rose Wanyonyi: Ningelipenda kuongea juu ya wamama. Wamama tuna shida nyingi sana. Jambo la kwanza ningelipenda hata sisi wamama tupewe uhuru wa kuongoe jambo lolote hata mbele ya wazee. Kwa sababu tumefinywa sana kwa njia nyingi.

Com. Lethome: Na leo ndio nafasi ya uhuru kabisa, sema vile unataka.

Rose Wanyonyi: Pili, ningelipenda serikali ikumbuke wamama ingalao tunateseka kwa njia nyingi. Tunapata shida hata jinsi unaweza nunulia mtoto uniform au kitabu unaona ni shida nyingi sana. Sasa serikali ikumbuke isaidie wamama kuwapatia kitu kidogo kama loan hata wapate nafasi ya kuuza mboga sokoni au kitunguu ama nyanya.

Lingine, watoto wetu wanateseka kwa njia nyingi, wengine wanakuwa raped tunapata watoto wengine wanapata mimba, lakini sisi kama wamama hatuna njia ya kujitetea.

Com. Lethome: Ngoja, watoto wa kike wakiwa raped unapendekeza serikali ifanye nini?

Rose Wanyonyi: Ichukue hatua.

Com. Lethome: Kama vipi kwa mfano mtu akirape afanywe nini?

Rose Wanyonyi: Afungwe. Ndiposa sasa wengine waone ya kwamba hata mimi nikitenda jambo hili ni mbaya sana nitafungwa.

Com. Lethome: Kama miaka mingapi hivi?

Rose Wanyonyi: Sita au saba.

Com. Lethome: Wakitia wasichana mimba?

Rose Wanyonyi: Tena akitia msichana mimba ninaona achukuliwe hatua kali, kwa sababu wengine wanaweza tiwa mimba wakiwa kama standard eight au wengine wako seven. Hata hawa watoto hawajui jinsi wanaweza kujisadia na watoto wao. Sasa sisi kama wamama tunapata shida nyingi kulea hawa watoto na hatujiwezi.

Com. Wambua: Hatua gani?

Rose Wanyonyi: Hatua ya huyo kijana kuchukuliwa pia ni kufungwa. Kwa sababu kuna wengine wanakataa hawa watoto. Wanawatia mimba na wakiambiwa wakuje pengine watoe mahitaji kwa huyo mtoto wanakataa msichana wanakataa na huyo mtoto pia.

Com. Lethome: Na akikubali kumuoa ama akikubali kumwangalia?

Rose Wanyonyi: Akikubali kumwangalia hapo tunaona tena inakuwa kama ni jambo lingine linaweza kuwa sawa. Na lingine tunaonelea kwamba hata sisi kama wamama ingelikuwa afadhali serikali kutupatia kama Ministry ya wamama, iitwe Women's Ministry. Sasa hiyo mahali wamama wanaweza kimbilia na kupeleka malalamishi yao. Asante.

Com. Lethome: Umesema kina mama wanapata shida ya kununulia watoto vitabu na vitu vingine vya skuli? Si ni wewe umesema hivyo? Ungependekeza nini ili hiyo shida iondoke, unapendekeza nini?

Rose Wanyonyi: Hapo niliongea ya kwamba serikali ingekumbuka kutupatia kitu kidogo kama loan, ili itutetee kwa kuuza vitu vidogo vidogo sokoni.

Com. Lethome: Asante Mama Rose. Tumpate mtu mmoja kabla ya kumsikiza Madam DO. Patrick Wambilianga?

Fr. Francis Sikisa: I will, I'll try. Thank you.

Com. Lethome: Thank you very much Father. Can we have now Oriama Benson. Na tujaribu kwenda haraka haraka sasa, Oriama. Watu ni wengi sana. We have over 200 people who want to speak.

Oriama Benson: Majina ni Oriama Benson. Nitaguzia mambo machache kidogo ambayo ninaona yanamguza mwananchi wa kawaida. Jambo la kwanza linaguzia ufisadi. Na nilikuwa ninaona kwamba kuweza kuepusha ufisadi katika utumishi wa serikali, nafasi kama madaktari ambao wameajiriwa na serikali wasiweze kuruhusiwa kuwa na biashara zingine kule kando.

Kwa sababu mara wakati mwingi wanatumia kuhudumia biashara zao na hawahudumii wagonjwa katika mahospitali. Madawa yanapotea mahospitalini kwa ajili ya kupelekwa katika biashara zao. Kwa hivyo wasiweze kuruhusiwa kuwa na biashara zao kule nje.

Pia jambo lingine ambalo ningependa kuguzia ni kuhusu Wabunge wetu ambao wako katika Bunge. Wako kule kwa ajili ya kumwakilisha mwananchi wa kawaida na tumeona kwamba Wabunge wengi hawafanyi kazi jinsi ambavyo inawapasa. Ningeomba kwamba katika Katiba yetu mwananchi wa kawaida aweze kuruhusiwa kama Mbunge hataweza kufanya kazi jinsi inavyompasa akaweze kuregeshwa nyumbani na pia akaweze kushtakiwa na agharamie by-election.

Jambo lingine ni kuhusu Rais wa nchi yutu pamoja na mawaziri. Tunapata ya kwamba kama Rais wa sasa anatumia wakati wake mwingi kutetea chama badala ya kutetea mambo ambayo yanahusu nchi yetu ya Kenya. Kwa hivyo Rais anapochaguliwa kama Rais aachane na mambo ya Chama na ashughulikie mambo yanayohusu nchi yetu. Hivyo hivyo likaweze kutendeka kwa mawaziri wetu pia.

Jambo lingine ambalo ningependa kugusia ni kuhusu jinsi ambavyo wamepoteza pesa. Ni pesa kiasi gani wamepokea na jinsi ambavyo wametumia. Kwa hivyo kila baada ya mwaka mmoja wakaweze kuelezea juu ya matumizi ambavyo wameweza kutumia hizo pesa.

Jambo lingine ni kuhusu msafara wa Rais. Tumeona ya kwamba Rais anaposafiri kwenda mahali, anakuwa na msafara mrefu na huo msafara kidogo unatumia fedha ambazo zinatoka kwa mwananchi wa kawaida.

Com. Wambua: Msafara wa magari ama wa watu?

Oriama Benson: Msafara wa magari na watu pia. Kwa sababu gari haliwezi kukimbia bila mtu. Kwa hivyo huo msafara ukaweze kupunguzwa ili kwamba fedha zinazotumika kwa huo msafara pia zikaweze kupungua.

Com. Wambu: Unapendekeza magari mangapi?

Oriama Benson: Ikiwa zaidi isizidi magari kumi.

Com. Lethome: Na wakati anaenda ng'ambo na ndege?

Oriama Benson: Akienda ng'ambo kama ni shughuli ambazo zinahusu Ministry ya Foreign Affairs atembee na Minister wa Foreign Affairs na Katibu wake. Lakini utapata kwamba mara kwa mara unasikia Minister asiyehusika na mambo ya ng'ambo, pia amesafiri. Kwa hivyo hiyo tunaona kwamba sio mzuri kabisa.

Jambo lingine ni kuhusu elimu: Tukienda katika shule zetu hasa shule za upili utapata kwamba kuna wanafunzi ambao wana wazazi ambao wanajiweza na wengine wazazi wao hawajiwezi kulipa karo. Lakini kwa vile wamepata katika shule moja huyu mwanafunzi asiyejiweza anapofukuzwa nyumbani ataketi pengine mieze miwili na akipata karo ya kuweza kurudi shuleni, analazimika kulipia ule muda ambao hajakuwa shuleni. Kwa hivyo analipia ule muda ambao hakuweza kuwa shuleni na zile services ambazo hakuweza kupata. Kwa hivyo kama kwamba itawezekana akaweze kuruhusiwa kulipa ule muda ambao atakuwa shuleni.

Jambo lingine ni kuhusu wafungwa wetu katika jela zetu. Wafungwa hawalindwi kwa njia ipasavyo. Mnasikia kwamba mfungwa akiwa mgonjwa hata kupelekwa katika hospitali inakuwa shida. Kwa hivyo kupata matibabu kidogo inaumiza ndiposa tunasikia wafungwa wamekufa katika jela. Kwa hivyo badala ya kuwarekebisha ili wakaweza kuwa wazuri katika jamii unasikia kwamba ameanga. Kwa hivyo sioni kama hapo tutakuwa tunawasadia. Badala ya kuwasaidia wakaweza kubadilika tunawasaidia kwa njia ya kuwaua. Kwa hivyo mimi naonelea kwamba mfungwa anapofungwa akaweze kupata matibabu wakati anasema kwamba ni mgonjwa.

Na pia ule uhamisho wa mfungwa kutoka jela moja hadi ingine. Unapata kwamba mtu amefungwa Bungoma kesho unasikia yuko Kodiaga, siku ya tatu unasikia amekufa kule. Kwa hivyo inakuwa ni mzigo katika jamii kuweza kuenda kubeba ule mwili wa huyu mfungwa kuweza kuleta nyumbani. Na kama itatendeka kwamba mfungwa amehamishwa na ameweza kuaga dunia mimi naonelea kwamba serikali ikaweza kugharamika, kumbeba huyu mfungwa kutoka pale ambapo amekufia, kuletwa nyumbani na pia gharama ya mazishi – nusu yake ikaweze kugharamika na serikali.

Jambo lingine ni kuhusu mawakili – advocates. Wamekuja kuwa watu waongo na wezi zaidi ya kiasi. Badala ya kusaidia watu ambao wamepatikana na cases kule kortini, unapata ya kwamba wanatumia hiyo nafasi kuona ya kwamba wanajinufaisha wao bila kusaidia huyu mtu ambaye yuko mahakamani.

Com. Wambua: Mtu mmoja ama wengine?

Oriama Benson: Wengine. Lakini sasa akiweza kusaidia hata hawa wengine pia wasipatikane naonelea kwamba kabla kesi haijaweza kukamilika huyu wakili akaweze kumuwakilisha huyu mshtakiwa na iwapo hiyo kesi itaweza kufaulu basi akaweze kulipwa pesa zake zote. Na mahali ambapo inahusika kwamba mimi ninadai pesa halafu yeye anapokea kwa niaba yangu isiwezekane kabisa. Pesa zikitolewa mimi nipate na nimlipe kazi yake. Na kama ya kwamba nitapoteza hiyo kesi kwa ajili ya uzembe wake, basi malipo yake yasiweko ama kama yatakuweko kwa sababu amekuja kortini alipwe nusu ya hizo gharama.

Jambo lingine ni kuhusu uhuru wa kuabudu. Naamini Katiba yetu ya sasa inaongea tu kwamba kila mtu yuko huru kuabudu. Kama utakimbia uchi ukijigamba kwamba unaabudu uko huru, lakini mimi naona kwamba Katiba itakayokuja ikaweze

kuangalia ni kiwango gani cha uhuru. Leo isipatikane kwamba mtu anaamka kivyake anasema ameanzisha kanisa fulani, na kwa vile Katiba inamruhusu kuabudu atasimama hivyo. Kwa hivyo tutafika mahali tuone kwamba tunapata njia nyingi sana za kuabudu ambazo hazifai kabisa. Kwa hivyo licha ya kwamba tutakuwa tunaabudu lakini kuwe na kiwango fulani cha kuabudu na wakati unaofaa. Isiwe tu kwamba utapata wengine tunapiga kelele zaidi ya kiasi, leo hapa tuko kwa bar dakika mbili zijazo watu wako wanahubiri na nini. Kwa hivyo kuwe na kiwango cha ule uhuru.

Com. Lethome: Dakika moja umalize.

Oriama Benson: Jambo lingine ni kuhusu wagonjwa ambao wamelazwa katika hospitali. Utapata kwamba mgonjwa amelazwa hospitali na ameweze kuaga either kwa uzembe wa wanaomlea katika hospitali ama wale madaktari na kama kwamba mgonjwa atapatikana ameaga kwa ajili ya uzembe wa madaktari, mimi naona kwamba zile gharama ambazo mgonjwa anahitajika kulipiwa zisiwezekane kulipiwa. La si hivyo wagawane gharama wale watu wa mgonjwa pamoja na hospitali.

Jambo lingine ni kuhusu hii habari ya appointment and re-appointment. Mtu leo amechaguliwa kwamba yeye ni chairman pengine wa Nzoia Sugar ameweza kufanya ulanguzi wa pesa kule, kampuni imeanguka anasimamishwa leo baada ya miezi mbili tatu mmesahau yale makosa alifanya, kesho unasikia pengine ameamkia kwa Lake Basin Development Authority. Kwa hivyo hilo jambo mimi naona kwamba hakika lisiweko. Mtu akishaappoint-iwa amefanya kosa, amefutwa ashtakiwe na abakie hivyo hivyo na aweze kugharamia kulingana na jinsi alivyokosa.

Jambo la mwisho kabisa ni kuhusu Commissions ambazo zinateuliwa na Rais. Hasa nikiambuka pengine zile ambazo zimetuliwa kwa ajili ya kuangalia tribal clashes, tangu 92 mpaka sasa. Naamini alipokea hiyo report na hatujasikia lolote kuhusiana na hiyo report. Kwa hivyo mimi naona kwamba once commission imeteuliwa imefanya kazi yake imemaliza na ime-hand over hiyo report kwa Rais, baada ya miezi miwili naamini atakuwa amepitia ya kutosha na akaweze kuiweka wazi na yeye akaweza kujua ni kwa nini ama ni mambo yapi ambayo waliweza kupata katika ule uchunguzi wao. Na hayo ndio mambo ambayo nimeweza kuwa nayo mchana wa leo. Asante sana.

Com. Lethome: Asante sana Benson.

Com. Wambua: Hawa maCommissioner wote ni mawakili.

Com. Lethome: Na sio wezi. *Laughter.* Tupate sasa, kuna mama yeyote ambaye alijiandikisha na hajazungumza, mama. Nyinyi Wabukusu mlizua kina mama kuja kuzungumza ama namna gani? Chief Henry Munyole? Tumsikize chief sasa.

Chief Henry Munyole: Mimi kwa majina naitwa Henry Munyole ni Chief wa Chwele location. Nitazungumzia hili jambo ambalo sisi sote tunahusika ni culture of violence ambayo imeenea sana katika areas zetu, utaona mtu anaamka anapiga bibi

yake hata anamuua ama anamuumiza zaidi. Mtu anaamka anapiga ndugu yake anamuumiza zaidi. Hiyo imetokea mara kwa mara. Iko rape cases nyingi na hizi zote mimi napendekeza ya kwamba P3 forms zikae na daktari ambaye anatibu huyo mtu. Zitoke kwa polisi ziingie kwa daktari. Na immediately yule mtu ambaye amefanya kitendo daktari akijaza hiyo P3 anashikwa mara moja na kushtakiwa.

Com. Lethome: Na hii mambo ya kupiga wanawake unapendekeza nini?

Chief Henry Munyole: Mimi nasema mambo ya kupiga wanawake isikuweco kabisa, hata kidogo. Kwa sababu mwanamke ako na akili unamuambia anaelewa. Kuna mwingine alisema ya kwamba ujue mimi nilikuwa nimeandika kuwe na mobile courts, lakini nimeambatana na yule alisema tuwe na traditional courts. Kwa sababu iko some petty cases ambazo hazistahili ziende kortini, zimaliziwe tu na wazee wa vijiji. Sasa tuwe na traditional courts. In most cases kuna mtu ambaye anaweza lease ng'ombe mtu. Naweza lease ng'ombe mtu na baadaye huyo ng'ombe auze kwa sababu ya shida yake. Kwenda kudai huyo ng'ombe anasema tuliandikishana wapi. Cases kama hizo sasa huyu mtu anaona hana ushahidi halafu ana resort kupigana, na tukiwa na hizo traditional courts hii itasaidia sana.

Tuko na trial marriages ambazo tunataka we discourage that one. Tuko na watu wengi anaoa bibi akizeeka tu kidogo anafukuza na watoto wote. Unaona hawa watoto wanateseka.

Com. Lethome: Kuzeeka ni miaka mingapi?

Chief Henry Munyole: Bora tu azae watoto kama watatu hivi ataonekana yeye amezeeka sana sasa anaenda kwa yule ambaye bado mchangamfu kidogo. Na huyu atatupiliwa mbali. Tuko nazo mingi sana nafikiri sasa Constitution yetu iseme ya kwamba ukioa bibi, maybe kumfukuza ni through the court. Lakini usiwe unaamka halafu unamfukuza. Wale watoto ambao wameachiliwa – abandoned children, tusaidiane wote kila mtu ambaye yuko kwa hicho kijiji akiona mtoto amefukuzwa na wazazi wake mtu yeyote ana jukumu la kuchukua atuletee mahakamani na mwenye mtoto ashtakiwe. Yeyote tu bora apate mtoto ako abandoned. Process ya kuenda through children office, Bungoma inachukua muda.

Inginge mimi napendekeza ya kwamba corporal punishment kwa shule zetu irudishwe, hiyo wasitoe. Watoto wetu wamekuwa wabaya na wakikosa shuleni achapwe kiboko.

Land transaction, kuuza shamba, ikiwa mtu anauza shamba mimi napendekeza ya kwamba vile mzee moja alisema kwa Land Control Board yule mzee wa ukoo – Land Chairman awe kwa board. Yeye pia athibitishie kwamba huyu mtu anauza shamba genuinely kwa reasons ambazo zimepeanwa. Kwa sababu wengine wameuza shamba na wamesubject families zao kuwa landless. Chairman wa clan awe kwa Land Control Board, yeye pia apeeane consent ya kwamba hiyo shamba imeuzwa.

Outdated traditions kama kutahiri wanawake, hiyo isiruhusiwe kabisa. Iambatane na Bwana Wamnyokoli hiyo ifutiliwe mbali.

Com. Lethome: Na ingine ambayo ni outdated?

Chief Henry Munyole: Outdated ni kama kurithi wanawake. Hiyo pia itupiliwe mbali.

Com. Lethome: Chief anatoa maoni yake.

Chief Henry Munyole: Upande wa security namalizia hii ya mwisho. Upande wa security tukiwa na insecurity hapa sometimes sisi kama administration tunakuwa na kazi ngumu sana. Naomba tu serikali iki-provide votes pengine ya kugharamia security within a certain area. Kwa sababu tumekuwa na majambazi wengi ambao wanafanya uhalifu. Sometimes we sacrifice we fuel the landrover or we hire a public vehicle ili kufukuza hawa majambazi ambao pengine wamepiga watu wetu. Kwa hivyo Government iki-provide certain funds itakuwa sawa sawa. Thank you very much.

Com. Lethome: Kuna swali.

Com. Wambua: Kuna pahali pengine tulisikia mambo ya akina mama wakipiga wazee. Sijui wewe kama chief umewahi kupata complaint kama hiyo? Umesema akina baba wasipige akina mama na hukutaja namba ya akina wazee ambao wanapigwa na ungelipenda kusema nini?

Chief Henry Munyole: Asante sana. Jambo kama hilo liko lakini it's very rare. Siwezi taja majina ya watu lakini kuna examples bibi ambaye alipiga bwana na alipiga baada ya kuvumilia. Huyu bwana baada ya kutoka amelewa akija na nyama yake anaweka hapo anakata vipande vipande na kipande anahesabu hivyo vipande hakuna kimoja ambacho kinaliwa. Moja iki-miss anapiga bibi na watoto. Sasa bibi wakaangalia siku moja wakaona huyu ni mlevi. Wakampiga sasa maybe out of protection, self-defence lakini kwa kimila yetu ya Wabukusu sijaona bibi akipiga bwana, it's rare. Pengine out of protection.

Com. Lethome: Maswali mawili kuhusiana na kwa sababu ya kazi yako. Hebu ngoja tumsikize kwa sababu ya kazi yako. Ya kwanza kuna watu wanapendekeza machief badala ya kuchaguliwa vile wanavyochaguliwa hivi sasa wawe yaani kuteuliwa sasa wanateuliwa wawe wanachaguliwa kama vile Mjumbe na Councillor wanachaguliwa. Sijui una maoni gani kuhusu hiyo. La pili, sijui kama ulikuweco, jana tulikuwa Sirisia na hapa Chwele na sehemu zingine za Kenya tumesikia watu wanasema local brews should be legalized. Hapa watu wako wanasema wanataka busaa, waachie wakunywe busaa bila kuingiliwa na polisi. Wewe kama chief tungenda utoe maoni yako, pendekeza.

Chief Henry Munyole: Swala la kwanza liko namna hii. Wananchi wanafikiria pengine chiefs wako na privileges nyingi, lakini for example mimi kama tawala chief kuteuliwa ni kama election na nahudumia watu wengi sio eti watu wa Chwele peke

yao. Mwingine anaweza toka Mount Elgon anadai huku kitu chake pengine msichana wake, pengine pressure pump amepeana mtu na imepotea na mimi mtu ambaye anapigia mimi kura na mtu wa Chwele. Sasa mimi kitu ambacho nafanya kwa vile sitaki nipoteze kura yangu, mimi nasema tu hakuna kitu chako hapa na anaenda, na kumbe ng'ombe wake ako upande huu. Siwezi kufanya haki, kwa sababu nikifanya haki nichukue ng'ombe mtu atoke Mount Elgon anakuja hapa anadai ng'ombe na mimi nichukue ng'ombe nipeane niko napoteza kura yangu, hiyo haiwezi fanyika hiyo.

Com. Lethome: Hebu nyamazeni tafadhali. Sikizeni haya maoni.

Chief Henry Munyole: Ingingine tuko na maybe application of cases. Nikiona ya kwamba huyu mtu ni my supporter na ako na dispute na aje mbele yangu. There is no way I can rule in his favour kwa sababu niki-rule in his favour hatanipatia kura. Nitaona ya kwamba wananchi wenyewe watakuja kuumia wenyewe. Niko tu hivyo hakuna kitu ambacho nitafanya nipoteze kura yangu.

Com. Lethome: Hiyo tumesikia kwa hivyo wateuliwe vile wanateuliwa.

Chief Henry Munyole: Busaa, sisi tunafuata sheria ambayo pengine imepitishwa na Bunge, Parliament ikisema isiruhusiwe sisi hatuwezi kuwafuata.

Com. Lethome: Sasa wewe zungumza kama Mbukusu. Usizungumze kama Chief. Hebu nyamazeni tusikie.

Chief Henry Munyole: Mambo ya busaa kwa sababu nchi yetu iko mbioni nasi tunataka maendeleo sio kuingilia tu busaa kwa sababu nchi yetu iko mbioni kila kitu ni competition. Tunataka watoto wetu wasome. Na ukiangalia area ambayo pengine tumependelea tu kunywa busaa hapa hakuna maendeleo.

Com. Lethome: Unapendekeza nini wewe?

Chief Henry Munyole: Napendekeza ya kwamba hii busaa isikuweko.

Com. Lethome: Iendeleo kuharamishwa. Mtu akipatikana nayo anashikwa.

Chief Henry Munyole: Anashikwa. *Laughter.*

Com. Bishop Njoroge: Hii mambo ya mabwana kupiga mabibi kwa sababu umesema imeenea sana na wanaume ku-rape akina mama na wasichana na watoto. Ungetaka sheria iwekwe kwamba mume ambaye anampiga bibi yake ashikwe na ashtakiwe? Pili, mtu ambaye amemnajisi mtoto au mtu bila kupenda kwake unajua sheria inasema unaweza kufungwa miaka

saba lakini hiyo inaonyesha haitasaidia. Ungetaka hukumu gani ili kuzuia mambo haya?

Chief Henry Munyole: La kwanza, bwana kupiga bibi yake inategemea bodily harm ambayo imefanyika. Kama alimkatakata kwa panga hiyo pia anaweza fungwa hata miaka kumi akimkatakata kwa panga. Na akimpiga kwa fimbo pia magistrate anaweza angalia na jinsi ugomvi ulivyotokea anaweza kum-release depending the damages on the body. Anaweza kum-release ya kwamba hata ikiwa bibi alikuwa na makosa na pengine ilikuwa tu kama discipline magistrate anaangalia.

Com. Lethome: In other words, unasema kama alimpiga kwa sababu ya discipline inakubaliwa?

Chief Henry Munyole: Kiwango ambacho sio bodily harm.

Com. Lethome: Sawa. Mwanamke akikosa discipline bwana akubaliwe kumpiga lakini asiumize.

Chief Henry Munyole: Asimumize.

Com. Lethome: Sawa. Na bwana akikosa discipline apigwe na nani na hatutaki aumizwe lakini atandikwe acharazwe na nani?

Chief Henry Munyole: Mimi nilisema ita-depend na judgement ya magistrate.

Com. Lethome: You are not answering my question, when a woman misbehaves she should be disciplined by the husband lakini asiwe na bodily harm. Who should discipline the man when he misbehaves in the house?

Chief Henry Munyole: The person who must discipline the man maybe bibi anaweza kum-report kwa authority.

Com. Lethome: Sio bibi amtandike?

Chief Henry Munyole: Tunaangalia political make-up pengine bwana ako na nguvu bibi anaweza kumpiga na anaweza kumtandika na halafu bwana amshinde nguvu. Anaweza kumtandika anyway lakini bwana anaweza kumshinda nguvu. Na hiyo inategemea kiwango cha bodily harm. Saa ingine kwa mila ya Kibukusu kwa sababu mambo ambayo inaletwa pengine bwana kuchapa bibi ni unfaithfulness. Sasa kitu kama hiyo lazima bwana anaweza piga bibi na kiwango ambacho hawezi kumuumiza. Na bwana akiwa unfaithful.

Com. Lethome: Na bwana akiwa unfaithful bibi amfanye nini?

Chief Henry Munyole: Na bwana akiwa unfaithful kwa Kibukusu anyway we allow may be polygamy.

Com. Lethome: You know being a polygamist is different from being unfaithful. Those are two different things. Ama, you can think about it anyway. Kina mama kataeni kuzungumza shauri yenu. Haya. Thank you very much.

Chief Henry Munyole: Thank you very much.

Com. Lethome: Henry Wekesa. Halafu afuatwe na mama yeyote ambaye amejiandikisha anataka kuzungumza. Wekesa Henry. Hayuko? Haya tunaendelea tumpate Godfrey W. Murunga, KNFU Chairman. Murunga? Okay, welcome Murunga. Afuatwe na Cleofas Wayongo. Wayongo yuko? Okay, Wayongo utamfuata.

Godfrey Murunga: Kwa majina ni Godfrey Wafula Murunga, KNFU Chairman, Chwele Division. Nina maoni kuhusu hii Katiba mpya kwanza ningependelea hii nchi iendelee kuitwa Republic of Kenya. Kitu cha pili, aina ya serikali iwe aina ya majimbo. Na isimamiwe na Governors basing on provincial boundaries. Tuwe na Central Government vile vile headed by the President and he/she should be elected directly by Kenyans after every five years for not more than two terms that is 10 years. The person should be with a clean record who is not a criminal and must have been a resident for more than five years and a farmer, because Kenya is an agricultural country. He must not aspire for any other seat e.g. an MP or party chairman. The age must be between 35 to 70 years. We need to have a Prime Minister who will be elected by the Parliament. Appointments are as follows:-

(1) We need to have one man one job.

Com. Lethome: One woman?

Godfrey Murunga: One woman one job also. No more than that. The President should be given powers to appoint the Vice President but the President should not be above the law but should have power to hire and fire.

Uraia: Uraia ningependelea kuona raia wa Kenya awe kwa kuzaliwa, kuoa au kuolewa kwa kutuma maombi. Ukiishi hapa kwa miaka zaidi ya kumi lazima ujiandikishe kuwa raia wa Kenya. Kama mzazi ana kicheti cha kuwa raia mtoto wake automatically ni raia wa nchi. Tuwe na uraia mara mbili: wa nje na Kenya. Tuwe na uraia mahali mbili – Kenya na uwe at least na any other country. Uraia wetu uwe identified kwa kutumia national ID card na cheti cha uraia.

Ulinzi na usalama wa taifa: Ulinzi na usalama wa taifa ningependelea kuona hasa GSU, police na askari jela hivi vyombo vya usalama na matawi yake yaundwe na Katiba. Na tuwe na utaratibu wa majeshi na silaha kupitia kwa Bunge. Na Rais asiwe amiri jeshi, jeshi wasimpe uwezo wa kuwa amiri jeshi. Na Bunge lipewe uwezo kuamua juu ya kazi ya usalama wa nchi.

Vyama vya kisiasa: Vyama vya kisiasa ikiwezekana tuwe na vyama vitatu. Chama cha kutawala na vyama vya upinzani viwili. Na vyama hivi vigharamiwe na fedha maalum kutoka serikalini.

Miundo na aina ya serikali: Kwa upande wangu naona tukiendelea kufuata tuwe na muundo wa aina ya mseto ambapo mamlaka ya nchi yamegawanywa, baina ya Rais na Waziri mkuu. Igawanywe kulingana na wingi wa kura na uwezo wa vyama.

Na upande wa Provincial Administration ningependelea kuona ya kwamba wenye viti hasa kutoka kwa sub-location mpaka district level wasimamie upande wa utawala, yaani Administration. Wapigiwe kura. Ukiwa mwenyekiti wewe usimamie kulingana na area ile umechaguliwa.

Bunge: Bunge iwe ikiendelea kila siku, working days from Monday to Friday, isiwe na siku mbili tatu na wanalipwa pesa nyingi. Waendeleo throughout the week – weekdays.

Na umri wa Rais ikiwezekana uwe between 35 to 70 years asiwe chini ya hiyo. Na wananchi wawe na uwezo ya kumregesha nyumbani Mbunge baada ya every after five years only – miaka mitano ikiisha ndio wananchi wana uwezo wa kumregesha Mbunge.

Com. Lethome: Kama vile ilivyo sasa.

Godfrey Murunga: Kama ilivyo sasa. Na Wabunge wafanye kazi kwa uaminifu kwa vyama vilivyowateua. Mbunge akipinga chama ambacho kilimteua automatically a cease kuwa Mbunge wa hicho chama. Apinge chama chake akiwa nje ya chama asiwe ndani ya chama, ili tuingize watu wengine.

Na upande wa gender, upande wa wanawake kuteuliwa mimi ningependa kusema wanawake hapa Kenya ndio wengi kushinda wanaume. Ni heri wanaume wateuliwe kwa maana wanawake wapiga kura wana kura nyingi kutushinda.

Hapa ninaenda kwa upande wa mamlaka ya nchi. Kwa maana kulingana na nchi yetu ya Kenya mamlaka ya nchi yamo mikononi mwa Rais. Lakini Katiba hii tupewe mamlaka Bunge iwe na mamlaka yote badala ya Rais kuwa na hayo mamlaka. Na ikiwa umepita kura uende kwa vipindi viwili tu hata uwe Mbunge, uwe Councillor ama uwe Rais vipindi viwili is enough uende retire.

Interjections: Inaudible

Godfrey Murunga: Five years kwa vipindi viwili yaani 10 years iwe maximum. Na unaenda retire. Bila makosa ulipwe

pension, ikiwa na makosa hakuna pension upoteze.

Na upande wa haki ya ardhi na mali hiyo ndiyo itakuwa ya mwisho. Ningependa swali ambalo liko ni nani anayepasa kuwa mmliki wa mwisho wa ardhi? Mimi nasema ardhi imilikiwe na jamii ya mahali pale. Na upande wa ardhi, je kuwe na kiwango cha juu cha ukubwa wa ardhi inayoweza kumilikiwa na mtu binafsi? Mimi nasema ndio. Iwe ili kila mwananchi apate haki yake ya kumiliki ardhi.

Com. Lethome: Eka ngapi lakini?

Godfrey Murunga: They divide according to the population of the country, ili kila mmoja awe ana haki ya kumiliki shamba.

Com. Lethome: No, umesema kuwe na kiwango cha juu, eka ngapi?

Godfrey Murunga: Ile ya juu isipite hekari kumi, maana wengi wana maelfu ya eka na hata hailimwi. Wanaume na wanawake wawe na uwezo sawa wa kumiliki ardhi. Hii swali kwangu mimi nasema haiwezekani. Kwa maana kulingana na kwetu hapa mwanamke huwa anaoleka akiolewa nje anaitwa mali ya mwanamume. Kwa maana mwanamume huwa analipa mahari na akiondoka kwa upande alizaliwa inaonekana it's minus hawezi kupewa kitu tena huko. Sasa umilikaji ikiwa tunataka iwe sawa mwanamke asiroleke na alipiwe mahari. Na shamba aende na shamba ya bwana, bwana awe na shamba waweke pamoja ndio tuwe na haki ya umilikaji.

Com. Lethome: Sasa unazungumzia habari ya mwanamke unazungumzia habari ya yule msichana ambaye anaolewa anaenda.

Godfrey Murunga: Ndio.

Com. Lethome: Na yule ambaye haolewi kwa sababu sio lazima. Kwanza ni hatia mwanamke kukosa kuolewa? Is it a crime?

Godfrey Murunga: No, no it isn't.

Com. Lethome: So she can decide not to marry.

Godfrey Murunga: Correct.

Com. Lethome: So what happens to this lady who is not married?

Godfrey Murunga: Mimi nasema ikiwa mwanamke hajaoleka na amekaa kwao na ana umri wa zaidi wa miaka hamsini huyo awe considered kupewa kitu. Lakini akiwa msichana bado hiyo itakuwa kugonganisha mahali ataoleka.

Com. Lethome: Watoto na bibi yako nyumbani ana haki ya kumiliki hiyo shamba ama? Yule ambaye umemuo. Mama ya hawa watoto.

Godfrey Murunga: Bibi yangu ni mali yangu. Na mimi nikiondoka watoto wangu watamiliki na mama yao atakuwa na faida.

Com. Lethome: Atamiliki ama hamiliki mama?

Godfrey Murunga: Kulingana na mimi na desturi na kimila yetu, mwanamke hana haki hata kidogo ya kumiliki shamba ila tu kupitia kwa mtoto wake.

Com. Lethome: Yaani yeye atapata faida tu ya ile shamba, lakini hawezi kumiliki? Title haiwezi kuandikwa kwa jina lake?

Godfrey Murunga: Haiwezi. Haiwezekani. Ikitoka kwangu inaingia kwa majina ya watoto wangu.

Com. Lethome: Wa kiume?

Godfrey Murunga: Wa kiume. Na tena hapa ningependa kumaliza hivi, upande wa mashamba ya marehemu ikiwa baba mzazi ameaga dunia tunaonelea mashamba ibadilishwe tu kwa majina ya watoto bila upingamizi wala gharama yoyote. Watoto wana haki ya kumiliki shamba la mzazi wao ambaye ameaga dunia na mambo ya kugharamia mimi naona inamalizia watu muda, tena inafanya wengine wameshindwa kubadilishiwa hiyo. Ikiwezekana wapewe. Malipo yatoke na ni ya juu sana.

Halafu ya mwisho, mimi nikiwa Chairman wa KNFU, waalimu wana chama chao kinaitwa KNUT. Na KNFU ina haki kwa mkulima. Ningependelea wakulima wote kupitia kwa ma-society zao na kila mahali wawe automatic members wa KNFU, bila kuwatoa nje. Asanteni. Thank you very much.

Com. Lethome: Ngoja kidogo, kuna swali hapa.

Godfrey Murunga: Uliza tu.

Com. Wambua: Mzee akifa na awe hakuwa na watoto wa kiume bado unasema mama asipewe au asirithi shamba, linaenda wapi?

Godfrey Murunga: Kulingana na mimi shamba ni la ukoo na ikiwa shamba ni la ukoo hata mimi nikifa ama mtu yeyote wa kiume akifa, hilo shamba ukoo ndio una uwezo wa kujua the next of kin. Kama ni mama ukoo una uwezo wa kumpatia. Kama sio mama lazima watajua ni yupi, hata kuna wengine akiona anaenda kufa na hana mtu wa kurithi, mambo ya Will vile vile ina umuhimu wake. Nadhani hiyo tutahimiza watu waelewe, akikosa mtoto na ajue mambo ya kupeana Will. I think it is like that.

Com. Lethome: Katika President umesema awe resident for more than 10 years, ama sivyo?

Godfrey Murunga: Five years.

Com. Lethome: Five years?

Godfrey Murunga: Yes.

Com. Lethome: Ninaweza kuwa mimi ni m-Tanzania au ni m-Ganda nimekuja Kenya nimekaa for five years, do I qualify to vie for Presidency?

Godfrey Murunga: Kwa utangulizi nilisema lazima awe mkulima na mkulima atalima wapi? Lazima alime kwa shamba ya Kenya na awe amepata hilo shamba kulingana na registration.

Com. Lethome: Okay nimekuja kutoka any country nimenunua shamba langu hapa, nimeanza kulima kwa hivyo nimekuwa mkulima nimefikisha miaka mitano. Do I qualify to vie for Presidency?

Godfrey Murunga: No. It's a capital NO.

Com. Lethome: Why?

Godfrey Murunga: Wewe ni mgeni.

Com. Lethome: Kwa hivyo the issue is not resident, he should be a citizen? Not resident?

Godfrey Murunga: Yes, that's why I put it there to be registered.

Com. Lethome: Unajua resident is different from citizen?

Godfrey Murunga: Correct. Thank you. Any other?

Com. Lethome: Haya asante Bwana mzee tumepata mambo mengi. Kuna mama yeyote ambaye anataka kuzungumza. Mama baada ya mzee utazungumza wewe mama. Halafu huyu mama akimaliza yule mama mwingine pale hivi. Hii ndio fursa mko nayo kuzungumza sio msem tukishaenda, sasa ndio nimekumbuka, ukikumbuka tutakuwa tuko Nairobi saa hiyo haitakusaidia.

Cleofas Wayongo Musee: Mimi kwa majina ni Cleofas Wayongo Musee. Mimi niko hapa na memorandum yangu kidogo ambayo nitajaribu kusoma.

Com. Lethome: Usisome yote.

Cleofas Wayongo Musee: The recommendations that I have here are very few they are not many. The first recommendation is concerning the President. The powers which have been given to the President are so much that he has been interfering with the powers of Parliament, when it should be independent. The elected people such as Members of Parliament and Councillors are directly elected and are denied meaningful role in administration. Instead he appoints people like the PCs, the DCs, the Chiefs and so on and these ones they are answerable to him and will not really help the citizens of the country. I therefore propose here that because of such powers, the Provincial Administration should be removed and be replaced by elected people for:-

- (1) Corruption in this country has become too much because of Provincial Administration, because it has been given a lot of powers and therefore they can do anything they like. Secondly, now this is the colonial era which was there and therefore it must be abolished.
- (2) I propose that we should have Coalition Government instead of the present Government that we have, so that the people of Kenya can be able to enjoy the freedom of independence instead of frustrations that are there within one party. I also propose that the disabled people in Kenya should be treated as any other Kenyan. I also propose that all customary by-laws of every tribe in Kenya should be maintained. For example, Wabukusu's by-laws such as circumcision, dowry settling and so on should be respected. And all ceremonies that are done by Wabukusu is always done by brewing beer that is busaa, which should be respected.

Com. Lethome: I believe that means should be legalized.

Com. Wambua: Are there some customs which you consider that should be done away with if we were to come up with a law which respects certain values like human rights and so on and so forth? Or are you saying that wholesale because yesterday we heard at another point in Sirisia that the Teso would want to be given their right to exhume their bodies and that

could offend the Bukusus. They said they should be given a right after three years to exhume the bodies and put the bones somewhere. Are there customs which you think we should do away with or must we say blanket all customs to be respected however offensive they are and we preserve them?

Cleofas Wayongo Musee: No if there is a custom that can affect the people, now that one is a different case but if there is nothing of that kind, then our customary laws should be respected.

I also would like to suggest that agricultural inputs which are now very high, the prices should be reduced immediately so that to allow the farmers to grow enough food for export and use at home. This I say because you will find that we always buy fertilizer at the price of around Shs.1,500/= that is one bag, but when we sell our maize when we go to the maize seed we buy it at 1,000/= around 400/= and after we have grown these maize and then we want to sell one bag, it only costs about 400/= which means the farmers are really suffering.

Com. Lethome: Okay we get the point. Go on.

Cleofas Wayongo Musee: I also suggest that the 8-4-4 system which has been there for long should be abolished and be replaced by the old system. Now all people should be set free to drink without interference.

Com. Lethome: Drink without interference.

Cleofas Wayongo Musee: Without interference because when you interfere with people that is the time when people get many crimes, but when people are set free you will find that most of the people will not really be affected in any way.

Com. Lethome: Excuse me, you know when you talk about people to be allowed to drink freely, I don't know whether you read in the papers or may be you heard it in the electronic media sometimes back watu walikunywa wengine wakakufa, wengine mpaka leo hawana macho, macho yamepotea. Sasa are you talking of that absolute freedom to drink anything, any poisonous drink?

Cleofas Wayongo Musee: Not anything. This is the drink which has been examined that one there can be said to be..

Com. Lethome: Busaa.

Cleofas Wayongo Musee: The brewer is the one that has to be examined.

Com. Lethome: Even that kumi kumi was also examined by the brewer. The person who brewed that kumi kumi that killed

people had examined it. It has not been examined properly that is why it killed people. In other words you are saying legalise busaa. Busaa should be legalized.

Cleofas Wayongo Musee: That one should be legalized.

Com. Lethome: Okay.

Cleofas Wayongo Musee: Now the duration of the President should be 10 years and the appointment of the President should be from 50 years onwards and the maximum should be 75. Now I also would like to talk about the salaries in Kenya because now that the economy has dropped and somewhere other people are getting a lot of money, so I propose that the minimum salary of every Kenyan should be K.Shs.10,000/= . And the companies in Kenya whereby the President has been appointing the Chairmen and so on, this one here should be appointed by the millers themselves and then be confirmed by the Members of Parliament. Thank you.

Com. Lethome: Thank you very much Cleofas. Moses Nandasaba. Oh, mama, mama. Halafu mama wawili, kisha Moses Nandasaba yuko. Haya, Moses utafuata hawa akina mama wawili. Haya, mama sema jina lako halafu uendelee.

Victoria Muyekho: *Esie ndaloma lubukusu. Nitaongea Kibukusu.*

Com. Lethome: Our Bukusu translator. She is Victoria who?

Victoria Muyekho: *Esie ndikho nomalomanga nga mayi*

Translator: I am speaking as a mother.

Victoria Muyekho: *Bindi bibie embona khulondakhano nde tsiloni nitso sirikali ilananga*

Translator: According to the loans given by the Government.

Victoria Muyekho: *Bakhasakhulu befwe bano babukulanga nga emikundu nibatitirira tsiloni mana efwe khuli nende abaana engo*

Translator: Our husbands are taking title deeds as security for loans and yet we have children at home.

Victoria Muyekho: *Esie nga mayi nende abaana sindamanyirekho da*

Translator: Without consulting us.

Victoria Muyekho: *Nono ngababukula tsiloni tsola abundu bakhirwa khurunga*

Translator: And when they are unable to pay.

Victoria Muyekho: *Mala efwe khumiya nende abaana bakhwangata khubarabara khukorwa khucha waena ta*

Translator: We are thrown out of our land and thrown on the roads and we don't know where to go.

Victoria Muyekho: *Malanga khutsa wakhubolera bari khotsa khumasa khotsa wasubchief mala ngabakhurebewo somanyirekho nolia ota okhutsiba ta nono esie embola ndi ebindu biakhutirira kumukunda elino barusiekho*

Translator: I recommend that the question of taking title deeds as security be removed.

Victoria Muyekho: *Namwe kabali sibakhola barrio ta balanga a family yosi ibewo niye babukula omukunda okwo*

Translator: If that title deed has to be involved then the whole family should be involved before it is taken as a security.

Victoria Muyekho: *Sikira efwe kata khwola abwenowo aba ngesie nga mama khwira nga nelomaloma malaba omusakhulu wachira ta okorwa wetsile mutown mala efwe khukhwirwa oli ocha khubarebe bakhwikana nono efwe khutsa wayi*

Translator: When we are dumped into danger the man takes off and now as a mother I am left without anywhere to consult and nobody to go to.

Victoria Muyekho: *Halafu likhola khabiri esie ndikho nemanoma khulubeka lwa abaana befwe besikhana*

Translator: I am talking about our children – girl children.

Victoria Muyekho: *Abaana befwu basikhana balala khunyola khwebulwa mana khwalekha khwebula ne tsikhabi ta mala ngabatsa muchinju basacha batasisi ne khani mu family niye wamiremo olikho nende khumukunda khumulayi sefwe bandi serikali nganekholakha malaka kano ekhole eri abaana befwe bakhana boshi banyolakhasia ngawetsisi libosi ta.*

Translator: I am proposing that if our girls get a less fortunate marriage, they should come back and get a share in their original home however little it may be.

Victoria Muyekho: *Halafu babulirenge sa mayi balala bosu bali unfortunated khubera banyala bebula mala khwibulawo omwano omusolili ta bamayi benabo bosu ba be consider kho babakho ishare niye banyala babawo mupaka khunyangawe malirisia*

Translator: There are some mothers who may not be lucky to get boys, such a mother should also be considered to be given a portion that they may live on forever.

Victoria Muyekho: *Halafu lilondakho khulondakhane nende idawari esie nga mama ndamuchi khukhwe babukusu baninia tsikhafu tsakhira ta batsifu kumi na tatu ---- libe lilaka mbu nikhuli bari babungie tsikhafu tsibekho ngali tsikhafa munane nombakumi awo bakhayika ta*

Translator: I am recommending that dowry to be reduced to 8 or 7 animals.

Com. Lethome: Ngojeni wazee inaudible. Wacha mama azungumze. Haya endelea.

Victoria Muyekho: *Halafu kekhandi nikemberekho ninako*

Translator: The last one I have.

Victoria Muyekho: *Halafu limaririkha liamberekho nalio esie khulondakhana nende protection yefwe abandi befwu administration ---- balenjetanga khwamira khumakasa subchief assitant chief khubira olubekalwa malobanga nengachira khuloma ebindu bilala khumira nanga mala ne abaandu bana nibakhadiya khumanyira area niye wama ngalwamenyere namwa omenyere orie nata khunyala khwabona khunyanyasibwa lukali nono ne abandu bano esie mbayeresia pongezi endi bayendelea nende ikisi neyabwa eyo khubera banakhurukanga mungira ya khuloleshia nganomenyere Lundi nganoli lubeka khulondakhana nende efwe bamayi nende ifamily yefwe yokhuli ninayo.*

Translator: I am proposing that the Provincial Administration starting with the village elder to the chief because they are appointed with our problems they should continue that service, because without them we would have a lot of problems. They know our problems they have helped us, so they should continue.

Victoria Muyekho: *Halafu nimalirisia kabisa ndasaba ndi efwe bosu bakina mama bakhuwekho a ministry*

yakhalolereesie lubeka lweba bakina mama khuli nende butinyu bukali ata khubana befwe bakhana bali batiti khunyala khwanyola omwana bamukurwakho mala okhwirwa liaburura niye muche mwikhale mulomelome ebindu ebia bio esie siabange bakina mama bosu babekho nende ministry yabwe.

Translator: I am recommending that women get their own Ministry to address women problems especially the raping of girls and other issues, so that they can address those issues. That Ministry be known for women and deal with women affairs.

Victoria Muyekho: *Bulayi Muno*

Translator: Asante.

Com. Lethome: Ngoja kwanza. Swali kidogo. Kwanza mama kuhusu msichana ambaye hajaolewa kupewa shamba na baba yake, apewe ama asipewe? Au, msichana ambaye ameolewa halafu hiyo umesema akikosana na bwana yake akirudi nyumbani apewe, lakini nasema yule ambaye hajaolewa yuko pale nyumbani. Baba yake akifa wakati anagawia watoto wa kiume shamba ampatisie yule msichana ama asimpatisie?

Victoria Muyekho: Ampatisie.

Com. Lethome: Mtoto apatisie hata kama hajaolewa pale nyumbani.

Victoria Muyekho: Ndio.

Com. Lethome: Na kama ameolewa?

Victoria Muyekho: Kama ameolewa na anakaa vizuri hiyo hatushuguliki.

Com. Lethome: Okay, achukue huko kwa Bwana yake. Na kama Bwana ni maskini hana shamba?

Victoria Muyekho: Hiyo ni kuelewana na wazazi tu.

Com. Lethome: Aelewane na wazazi wake. Haya sawa. Na ungependa shamba title deed badala ya kuandikwa jina la mzee peke yake, iandikwe jina ya mzee na bibi yake pia ama namna gani?

Victoria Muyekho: Ningependa inandikwe jina la bwana yangu na watoto yake.

Com. Lethome: Na bibi?

Victoria Muyekho: Hata bibi lakini not very necessary. Ni watoto tu na baba yake.

Com. Lethome: Ngoja. Hii haitaki translation. Hii ni direct.

Victoria Muyekho: Inatakiwa tu watoto na baba yake.

Com. Lethome: Lakini sio bibi?

Victoria Muyekho: Sasa bibi anaingia namna gani? *Laughter.*

Com. Lethome: Okay, that's good. Tumesikia bibi akiwa amekosa nyumbani tumesikia maoni hapa inasema awe disciplined na bwana, bora tu asiumizwe. Si ndio? Una maoni gani wewe kuhusu hilo jambo na bwana akikosa discipline afanyiwe kitu gani?

Victoria Muyekho: Wamshtaki, atashtakiwa.

Com. Lethome: Na unakubali hiyo mambo ya mama kuwa disciplined na bwana? Kupigwa?

Victoria Muyekho: Hiyo mimi sitaki.

Com. Lethome: Haya asante mama. Enda ukajiandikishe jina hapo. Haya, yule mama mwingine karibu. Njoo tusikie maoni yako. Unataka kusema kitu, hebu mpatie aseme ile anataka kusema. Tumekuja kuzungumza na nyinyi na Walinywa tumekuja kuchukua maoni. Sasa wageni wakija kwa Wabukusu si Wabukusu mila yao ni wao ndio wanapatia wageni lunch? (Mai wange) Mimi ni mgeni ama si mgeni? (Nenya busuma). Haya sema jina halafu uendelee.

Irene Walubengo: Kwa majina ni Irene Walubengo.

Com. Lethome: Haya endelea Irene.

Irene Walubengo: Jambo la kwanza nataka kuongea juu ya masomo. Tunaona ya kwamba mtoto au mwanafunzi akimaliza kidato cha nne kama amefaulu kwenda kwa chuo kikuu yaani university hapo kuna pahali penye mwanafunzi anaruhusiwa kupewa loan na hapo Government ndio ilitoa hiyo kitu mwanafunzi kupewa loan ili aendelee na masomo yake. Na hapo inasaidia wale ambao hawajiwezi kuendelea na masomo yao. Lakini tunaonelea ya kwamba siku hizi kuna points ambazo

zimewekwa kama hujapata hizo points huwezi ingia katika chuo kikuu. Na kwa hivyo unaweza kosa ingine kwa chuo kikuu kama ulikuwa less by one point ama two points hivi. Na kwa hivyo hapo unaonelea hutaacha masomo lakini utajaribu ili uendelee kwa vyuo vingine kama polytechnic.

Sasa hapo mimi naona Katiba yenye inakuja pia loans zipewe wanafunzi wenye wanafua dafu kuingia vyuo vikuu kama polytechnic kwa sababu kuna wengine wenye hawajiwezi lakini walijaribu sana ili wafikie kile kiwango cha kuingia polytechnic.

Kwa hivyo naona kama hii Kenya kuna national polytechnics chache sana. Kwa hivyo mimi naonelea hizo polytechnics wapeane loans kwa wanafunzi wenye wamefaulu kuingia hapo.

La pili ni kuhusu introduction ya akina mama ama pia wababa. Unaona kama uko pahali wababa wanajitambulisha eti I am Mr. somebody halafu upande wa wamama kuna Mrs, Ms. na Miss. Sasa kwa hivyo unaona kama mwanamume ako tuseme 20 years anasema I am Mr. David somebody na hapo inamaanisha lakini mwanamke akiamka eti anajitambulisha anasema I am Miss or I am Mrs. Kwa hivyo hapo inamaanisha kwamba mwanamke huyo atajitambulisha na kwa kujitambulisha kwake itakuwa inaonyesha kwamba ameoleka ama hajaoleka.

Com. Lethome: Yaani anajulikana.

Irene Walubengo: Anajulikana hapo hapo, lakini mwanamume hatajulikana hapo hapo, kwa sababu yeye amesema tu I am Mr. na saa zingine ako 20 years na mwingine ako 50 ama 70 anasema I am Mr. Kwa hivyo mimi naonelea wanawake pia kama tunataka kujitambulisha tuseme tu kama mimi I am Irene Walubengo, tuseme tu I am Irene Walubengo sio Mrs ama Miss. Ibaki tu hivyo.

Com. Lethome: Jina la baba yako ama jina ya bwana?

Irene Walubengo: Hiyo niko naendelea ngoja kwanza. *Laughter.*

Com. Wambua: Endelea.

Irene Walubengo: Halafu tena sasa nakuja kwa hiyo upande wa jina la baba ama la mwanamume. Mimi naonelea wanawake hata kama umetoka kwa baba yako ukioleka kwa bwana ako utimize tu hilo jina la babako. Sitaki ile utumie la bwana yako. Natakikana kama mimi I am the daughter of Mr. Walubengo nibaki tu Irene Walubengo. Sitaki niende kwa pengine nioleke pahali pengine halafu nikiwa huko nibadilisha eti Mrs. Wafula. Hiyo ndiyo sitaki, kwa sababu leo kama hiyo ya kusema eti Mrs. Wafula, today I might be Mrs. Wafula but by 2004 I might be Mrs. Wanjala under sudden circumstances which can lead to divorce. Sasa hapo mimi naonelea kama mtu ameoleka aende tu huko, lakini jina tu la babake liendelee kutumia si la bwana yake.

Com. Lethome: Wasakhulu sikizeni mama anasema nini, maneno muhimu hii. Haya endelea.

Irene Walubengo: Halafu ya tatu vile walikuwa wanasema upande wa baba na mama kwa nyumba. Kama bibi amekosa ama eti bwana ampee punishment na je bwana naye atapewa punishment na nani?

Com. Lethome: Wewe unapendekeza nini?

Irene Walubengo: Mimi naonelea bwana kama bibi amekosa anaweza pewa punishment lakini unajua kuna different punishments. Unaweza mpea punishment kwa pengine kama alikuwa amefanya kosa kidogo hapo huwezi ukampiga. Hapo unamgombeza tu and that will also be a punishment. Lakini mimi siruhusu bibi apigwe eti kwa sababu amekosa. Kama jambo ni kidogo ni kuelewana tu kama bibi na bwana halafu muendelee kuishi. Lakini kama bwana pia amekosa si eti lazima umpeleke mbele, kwa sababu saa zingine bwana yaani kuna makosa ingine it is just a habit yeye kufanya hivyo. Sasa kama kosa kama hilo si eti lazima umpeleke mbele inatakikana pia yeye.

Com. Wambua: Makosa kama gani mama?

Com. Wambua: Baada ya huyu. Sasa...(inaudible).

Speaker: (?)

Com. Wambua: Sikizeni wazee ndio tumalize haraka. Sasa ni saa kumi na nusu na tukirudia maneno hapa yale yamesemwa tutakaa hapa mpaka saa kumi na mbili na hakuna haja. Kwa hivyo tutagawa wakati ndio kila mtu ataje jambo lake lile linamsumbua. Yale yametajwa tusirudie tafadhalini, tuchukue dakika mbili mbili tufunge kikao halafu nyinyi muende mukaangalie shamba, ng'ombe. Yule ambaye anataka kwenda kunywa busaa kama DO hayuko karibu, akanywe busaa. Tuendele. Dakika mbili Mzee, yale ya muhimu na kama yametajwa usirudie, tumepata yale na tutayaangalia, taja yale ambayo hayajatajwa.

Robert Wanyama: Kwa majina naitwa Reuben Wanyama. Nina machache kama yafuatavyo. Nitaanzia na uchaguzi wa rais wa nchi yetu. Ninaona huyu asiwe mwenye chama chochote cha siasa, awe neutral.

Com. Wambua: Imetajwa hiyo, endelea.

Robert Wanyama: Muda wake ofisini uwe miaka tano, kama amefanya vizuri afanye application tena na kama atafaulu aendele. Akishindwa, mwingine achukue, isiwe zaidi ya miaka tano. Kuteua rais, kuwe na kamati fulani ya kuchunguza wanaotaka kiti hiki na wawakilishi hawa wawili kutoka katika kila mkoa kuangalia maneno ya wanaotaka kiti hiki. Sipendelei rais yeyote akichukua hatamu kusema nitafuata aliyekuwa katika ofisi hii. Kuna mambo mengine wanasema watafuata na kumbe wanalipisha kisasi.

Com. Wambua: Sawa sawa hiyo tumeelewa.

Robert Wanyama: Sidhani ni vizuri. Awe na mambo yake na yawe mazuri. Aliyekuweko, yakiwa mazuri ayafuate na kama ni mabaya asiyafuate, kutoa kitu ambacho kinaitwa nepotism.

Com. Wambua: Lingine?

Robert Wanyama: Kwa education, waziri wa elimu anakosea wakati fulani. Watoto wa darasa la nane, matokeo ya mtihani yakitokea, anasema kiasi fulani cha watoto watapata nafasi katika shule za serikali na wengine hawataweza. Anataka hawa waende wapi?

Com. Wambua: Propose, unataka nini?

Robert Wanyama: Nasema aachie mzazi, yeyote ambaye mtoto amefaulu, kupata nafasi katika shule za serikali asiwe na pingamizi. Cost sharing imeumiza wananchi sana.

Com. Wambua: Hiyo imetajwa.

Robert Wanyama: Kutoka hospitali, watu wengine wanakufa nyumbani kwa sababu hawawezi hii cost sharing.

Com. Wambua: Hiyo imetajwa.

Robert Wanyama: Namalizia, watoto wetu wa miaka 18 na zaidi, wanajiona wao ni wazima na wakitaka kuo au kuolewa, wanatumia uwezo wao vibaya. Kama ni mvulana wangu anachukua msichana ambaye sijui na hata simfahamu na anamleta kama bibi yake na huu mzigo unakuja kwangu kama mzazi. Nilipe gharama ya mahari na kadhalika na kesho wanakosana na huyu msichana wake, nani anapata hasara? Napendekeza kwamba hawa wavulana na wasichana wetu, akipenda mpenzi wake, ajulishe mzazi na mzazi awe na la kusema na kama wanamuunga mkono, mambo yawe sambamba.

Com. Lethome: Wasipomuunga mkono?

Robert Wanyama: Wazo lingine liwepo.

Com. Wambua: Mzee asante sana.

Robert Wanyama: Hayo ndio maoni yangu.

Com. Wambua: Asante sana kwa maoni yako mazuri, tafadhali jiandikishe hapo, tumeyasikia. Mzee mwenzetu hapo afuate Richard. Ufupishe maneno maanake mengi yamesemwa, tupe mapya usirudie yale yamesemwa. Taja jina tena.

Richard Wasike: Richard Wasike na ningependa kupendekeza hivi; on the President, the immunity of the President must be

lifted in the constitution so that he faces the court of law (?). On the side of the President also, he should be able to be attending the parliamentary sessions so that he is able to answer various questions that are very touchy. On the judiciary side, I think the judiciary should be independent completely such that it should not be interfered with by the head of state in the event of officers performing their duty. The judiciary should have Judicial Commission that so far appoints them to that position they hold and because of that the President will not have powers to interfere with cases they oversee.

On political parties, we should have atleast 2 parties to avoid tribal parties in the country and causes confusion. All parties must participate in the development of the country. On the side of legislature, we have the members' salary in Parliament should be determined by the parliamentary commission which should not involve members as members of the commission, it should have an independent commission of parliamentarians to determine salaries. On the other side, we have those MPs who do not perform, should be recalled by the electorate. Members should be part-time to allow them time to attend to constituencies' issues.

Com. Wambua: Inaudible.

Richard Wasike: Yes. I should cherish the coalition Government. On education, I would recommend that the constitution provides the Government to give the textbook, i.e. the Kenya School Equipment Scheme should be revived and should be written in the constitution so that no body messes up with.... (inaudible).

Com. Wambua: Free education.

Richard Wasike: Yeah. I also want to recommend that the Government must provide employment to its people regardless of the race and it should not have any malice, fear or favour. On elections, there should be no defection from one party to another. Candidates who are elected, those who were once elected or not elected should not be allowed to switch to another party for (?). Seats in parliament should be reserved particularly for people like physically handicapped, women, etc. Election dates must be defined in the constitution, maybe let it not be part of the President.

Com. Wambua: That has been mentioned.

Richard Wasike: Thank you very much.

Com. Wambua: Asante sana Bwana Wasike kwa maoni yako mazuri, tafadhali jiandikishe hapo. Tufuate hapo na kama jambo limetajwa usirudie, leta yale ambayo ni mapya tumalize.

Jack Wamalwa Watibo: Kwa majina naitwa Jack Wamalwa Watibo

Com. Wambua: Jack?

Jack Wamalwa Watibo: Jack Wamalwa Watibo.

Com. Wambua: Endelea.

Jack Wamalwa Watibo: Maoni yangu napeana upande wa katiba isiwapo Kenya yetu, iondolewe mbali.

Com. Lethome: Katiba iondolewe mbali?

Jack Wamalwa Watibo: Iondolewe mbali.

Com. Wambua: Hakuna haja ya katiba.

Jack Wamalwa Watibo: Hakuna haja ya katiba.

Com. Wambua: Badala yake tuwe na nini?

Jack Wamalwa Watibo: Badala yake tuwe Wakenya watupu.

Com. Wambua: Bila sheria, bila katiba... (inaudible).

Jack Wamalwa Watibo: Tuwe na sheria na tutawaliwe na President akipenda watu wake wote.

Com. Wambua: Bila sheria bila katiba

Jack Wamalwa Watibo: Kupitia katiba, nimesema...

Com. Wambua: Kama unataka kufikiria, tutaweza kumpa mwingine nafasi, ufikirie kwanza halafu nitakuita baadaye.

Jack Wamalwa Watibo: Sawa.

Com. Wambua: Maanake inaonekana ni kama maneno yamepotea. Wacha tumpe mwingine nafasi. Fikiria tutakuita tu, keti hapo

Jack Wamalwa Watibo: Pole, kupitia kwa katiba mpya ama President, naomba tusiwache uhalifu utatize wananchi sana kwa sababu hii maneno ya uhalifu imeumiza wananchi. Hasa upande wa Pokot

Com. Wambua: Tupatie proposal tafadhali, pendekezo ni nini? Ugependa katiba iseme nini?

Kwanza umesema hutaki katiba, unataka nini wewe? Tupe proposal.

Jack Wamalwa Watibo: Hapo nilipotea, sio katiba, nilipotelea tu.

Com. Wambua: Sasa nataka proposal yako ni nini?

Jack Wamalwa Watibo: Nataka President alinde wananchi wake kwa umoja.

Com. Wambua: Hiyo tumeelewa.

Jack Wamalwa Watibo: Asibague.

Com. Wambua: Haya, next one. President alinde wananchi wake kwa umoja, asibague. Tuambie next point.

Jack Wamalwa Watibo: Upande wa kugawa mashamba, ikiwa anataka kugawa mashamba ikipatikana, achanganye, mwananchi wa Kenya ni Mkenya.

Com. Wambua: Hiyo tumeelewa, next?

Jack Wamalwa Watibo: Anaweza kutoka Mombasa na aishi hapa Bungoma.

Com. Wambua: Tumeelewa hiyo. Next one?

Jack Wamalwa Watibo: Upande wa Pokot, watu wakifika msituni wanaumiza watu na kuiba ng'ombe, hawalimi. Hiyo misitu igawiwe wananchi, wananchi wachanganywe.

Com. Wambua: Tumeelewa.

Jack Wamalwa Watibo: Nchi itulie kuliko kuvuka huko na bunduki.

Com. Wambua: Haya, tumeelewa. Next?

Jack Wamalwa Watibo: Kwa upande wa msaada wa ukimwi, naonelea watu wa ukimwi wapewe msaada.

Com. Wambua: Haya

Jack Wamalwa Watibo: Maoni yangu ni kwamba watu wa ukimwi wapewe chakula tu, wasipimiwe chakula. Wasipewe pesa halafu waongeze kuumiza wananchi kwa sababu wana pesa mingi.

Com. Wambua: Una jambo lingine?

Jack Wamalwa Watibo: Nafikiri hiyo ndio ya mwisho.

Com. Wambua: Asante sana, jiandikishe hapo tafadhali. Mzee fuata. Jambo kama limetajwa usirudie tafadhali.

Peter Wenani: Asante.

Com. Wambua: Tuambie mapya. Taja jina na uendelee.

Peter Wenani: Kwa majina naitwa Peter Wenani. Langu la kwanza nasema upande wa mkulima, ningesema apewe advance wakati anapopeleka kahawa yake katika mitambo, 15 shillings per kilo advance. Wakati wa clashes 1992, watu walikufa hapa mlimani na serikali haikuwalipa, ningependekeza hao watu wafuatwe na walipwe.

Com. Wambua: Haya, next.

Peter Wenani: Ninaloongeza ni juu ya wazee ambao wako 55 years and above, wazee hawa wapewe kitu cha kuwalinda katika maishani mwao.

Com. Wambua: Next.

Peter Wenani: Linalofuata ni juu ya waalimu, mtu akipewa promotion tafadhali, awe kazi yake ionekane ndipo apewe promotion wala si bure. Jina la 'chokora', naomba katika Chwele tafadhali, jina la chokora litupiliwe mbali kabisa katika Kenya. Litafanya wageni kutoka nje waseme ya kwamba watu fulani chokora wako mahali fulani. Chokora litupwe mbali kabisa.

Com. Wambua: Endelea.

Peter Wenani: Mtu akitoka chama na aunde chama kingine asipewe uwezo huo wa kuunda chama kwa sababu yeye anataka kuchokora serikali hii.

Com. Wambua: Hilo limetajwa, endelea.

Peter Wenani: Mtawala yeyote akipewa, kwa mfano kama DO akipata transfer aende, mambo ya kusema kwamba wazee, ‘changa kitu kidogo kwa maana DO wetu anaenda’ isiweko.

Com. Wambua: Endelea.

Peter Wenani: Wakulima wa mahindi, mambo ya gorogoro itupiliwe mbali na serikali ilete store ili watu wajue jinsi ya kufanya kazi yao kwa shamba.

Com. Lethome: Gorogoro ni nini?

Peter Wenani: Gorogoro ni ile kitu ya kupimia mahindin, mtu akija ananunua hapo ya kupima

Audience: Two kilos.

Peter Wenani: Two kilos, ule mkebe tafadhali uondolewe na serikali itupatie ma-store ya kulinda ... (inaudible). Kitu cha mwisho ni juu ya rumande yaani jela. Na-recommend jela iwe safi, chakula safi, matibabu yawekwe halafu mtu hata ingawa ana taabu, apate maisha mazuri. Ni hayo tu.

Com. Wambua: Asante sana. Hiyo ya mwisho ilikuwa imetajwa lakini tumeisikia tena. Jiandikishe hapo.

Peter Wenani: Asante sana.

Com. Wambua: Asante sana. Sasa watu wasiongezeke, tutamalizia kwa huyo mzee ambaye ako na kofia hapo, hao ndio tulihasabu mwisho. Taja jina na uendelea.

Joseph Kimakuti: Kwa majina naitwa Joseph Kimakuti.

Com. Wambua: Joseph?

Joseph Kimakuti: Kimakuti.

Com. Wambua: Endelea Kimakuti.

Joseph Kimakuti: Jambo la kwanza ni kwamba nataka tuwe na uhuru wa kuabudu.

Com. Wambua: Limetajwa hilo, freedom of worship.

Joseph Kimakuti: Ningetaka kutoa mfano halafu ni-single moja halafu nizungumzie hii.

Com. Wambua: Freedom of worship is what you are proposing. Nimesema tafadhali, nitakupatia muda na tusiharibu muda na nikasikia hapa watu wanasema hiyo freedom of worship isiingize devil worship. Kwa hivyo kama unataka kugeuza hayo tupatie mapya, kama ni hayo hayo wacha tu na uendelee na jambo lingine.

Joseph Kimakuti: Jambo lingine, wale ambao wanafanya biashara ya jua kali, pendekezo langu ni kwamba watu ambao wana stock ya 50,000 and above wapewe license lakini 50,000 and below wafanye biashara bure.

Com. Wambua: Fifty (?)

Joseph Kimakuti: 50,000 and below wasichukue licence, wafanye biashara bure. Jambo lingine ni kwamba watu ambao wana miaka 60 kuenda juu, kwa mfano kama wanakosa kosa ndogo, askari asiende kwake na pingu. Aende amuambie polepole kwa sababu old age inasababisha shida.

Com. Wambua: Imetajwa hiyo.

Joseph Kimakuti: Okay. Jambo la tatu ili kupunguza ukimwi, vijana waweze kuwa examined. Chini ya hiyo ni kwamba wanafunzi wa shule, primary na secondary wapewe penalty ama prosecution, akipatikana akifanya mapenzi. Jambo lingine ni kwamba wale ambao wana virusi vya ukimwi, mtu mzima akipatikana akifanya mapenzi na innocent party aweze kushtakiwa. Lingine ni kwamba madaktari, ninapokufa kwa ukimwi hospitalini, waweze kutoa certificate kwamba nimekufa ukimwi na administration waje nyumbani na kutangaza kwamba huyu amekufa ukimwi ili uweze kupungua.

Jambo lingine, naunga wale walisema serikali iwafunze. Kuongezea, serikali iwape mashamba.

Com. Wambua: Okay (?)

Joseph Kimakuti: Kuhusu afya tumeona kwamba mtu anakufa kwa veranda kwa sababu hana pesa ya kumuhudumia. Kwa hivyo daktari ama nurses ambao wana kiburi, abuses na mistreatment, negligence ya kazi na mtu akufe pale, waweze kushtakiwa. Jambo la mwisho ni kwamba, customary law ya Wabukusu ni kwamba ng'ombe 13. Ninapropose ziwe sita.

Com. Wambua: Za nini tena?

Joseph Kimakuti: Customary law.

Com. Wambua: (?) dowry?

Joseph Kimakuti: Yeah.

Com. Wambua: Una-suggest 6 cows?

Joseph Kimakuti: From 13 to 6.

Com. Wambua: Asante sana, jiandikishe hapo. Taja jina na utuambie mapya.

John Walabamechi: Majina yangu ni John Wamalabe Mechi.

Com. Wambua: (?)

John Walabamechi: John Wamalabe Mechi.

Com. Wambua: Ngoja kidogo tafadhali. Mzee nilikuambia uje hapa, sijui, ulizungumza?

Speaker: (?)

Com. Wambua: Ushazungumza wewe?

Com. Lethome: Because you have been here since morning.

Com. Wambua: Kuja hapa. Huyu Mzee.

Com. Bishop Njoroge: Wewe mzee umekuja sasa hivi?

Speaker: Eh.

Com. Bishop Njoroge: Ni wewe ninazungumzia.

Speaker: Eh.

Com. Bishop Njoroge: Si umekuja asubuhi?

Speaker: Eh.

Com. Bishop Njoroge: Haya, ingia pale.

Com. Wambua: Wacha sasa tuone vile tutaelekea. Mzee utafuata, namba two, number 3, number 4, number 5. Tulikuwa tunaishia hapa, sijui hawa wametoka wapi wengine.

Audience: (?)

Com. Wambua: Number six, seven, eight, nine, ten, mwisho. Mtu wa mwisho hapo ni mwenye kuvaa shati nyeupe, amesonga hapa awe namba seven lakini yeye ndiye wa mwisho. Kwa hivyo tuelekee hivyo basi. Tuambie yale ambayo hayakutajwa na una hakika hayakutajwa.

John Wamalabe Mechi: Yale yenye.... (inaudible).

Com. Wambua: Jina?

John Wamalabe Mechi: Jina ni John Wamalabe Mechi.

Com. Wambua: John?

John Wamalabe Mechi: Wamalabe Mechi.

Com. Wambua: Endelea.

John Wamalabe Mechi: Nitataja yale yanahusiana na maisha yangu vile ninavyoishi hapa kwa nchi hii.

Com. Wambua: Endelea, unapoteza muda sasa.

John Wamalabe Mechi: Hapo nimeona wazee..... (inaudible).

Com. Wambua: Na ulete hiyo mic karibu.

John Walabamechi: Wazee walikuwa wananiambia hadithi ya kwamba mashamba walikuwa wenyewe wanajikatia tu halafu baadaye serikali ikaona ilete map ifanye survey kwa sababu watu wangechokozana na kusongesha. Waliendelea kuishi hii maisha rahisi tu. Tangu tuzaliwe, saa hii shamba ni tatizo ngumu sana, hata afadhali uwache shamba ukae tu uitwe chokora vile walisema. Ni ngumu sana na hiyo sheria irekebishwe.

Com. Wambua: Unataka nini?

John Walabamechi: Kwa sababu ukienda... (inaudible).

Com. Wambua: Unataka tufanye nini?

John Walabamechi: Nataka ikiwa mimi hiyo shamba ya baba nipewe na niwe na uhuru wa kukaa pale. Nisiwe na mambo mengine ama ndugu wanisumbue wakisema huyu hakuwa ama nini. Kwa sababu ukienda kwa serikalii wanasema toa pesa na mimi sina pesa.

Com. Wambua: Okay, endelea. Jambo la pili?

John Walabamechi: Jambo la pili, nilivyo hapa Kenya, nina ID card ya kujitambulisha mimi ni mwananchi asili lakini ningomba hii katiba ya kwamba watawala wetu watufunze sheria zingine, wasituangukie tukifanya makosa tu na hujui ama wafanye matangazo ati kupita mahali hapa ni hatari ili tuhepe. Tunatembea kwa giza tu.

Com. Wambua: Okay, next?

John Walabamechi: Ni hiyo tu.

Com. Wambua: Asante sana Bwana John, jilandikishe hapo, tumesikia na kupokea maoni yako. Taja jina Mzee, wewe ndiwe nimesikia umengojea sana.

Moses Kimakuti: Yes, mimi... (inaudible).

Com. Wambua: Kwa kuwa umengojea, usikae sana kwa kuzungumza mengi.

Moses Kimakuti: Nitafupisha.

Com. Wambua: Fupisha.

Moses Kimakuti: Kwa majina naitwa Moses Kimakuti.

Com. Wambua: Kimakuti?

Moses Kimakuti: Yes. Mengi yametajwa ijapokuwa nilikuwa napendekeza hivi, mbunge yeyote akichaguliwa na havezi kutekeleza jukumu la wale walimchagua

Com. Wambua: Anarudishwa.

Moses Kimakuti: Arudishwe.

Com. Wambua: Hilo limetajwa Mzee.

Moses Kimakuti: La pili, suspect should not be tortured by police.

Com. Wambua: Hilo limetajwa.

Moses Kimakuti: La tatu, counting of votes should be done at the polling station.

Com. Wambua: Limetajwa hilo.

Moses Kimakuti: Ni hayo tu. Asante.

Com. Wambua: Thank you very much Moses. Mambo yote hayo yako yaliingia. Jiandikishe hapo please. Taja jina Mzee na utuambie mapya tafadhali.

Henry Nyongesa Wanasamba: Kwa majina naitwa Henry Nyongesa Wanasamba.

Com. Wambua: Henry Nyongesa?

Henry Nyongesa Wanasamba: Henry Nyongesa Wanasamba.

Com. Wambua: Endelea.

Henry Nyongesa Wanasamba: Langu ni hili, mimi ni Mwanakenya na nimekaa hapa Kenya tangu mwaka wa 1951 mpaka saa hizi. Vile mimi naonelea, serikali yetu sio mbaya na langu nasema hivi, kama vile muko hapa, mukienda huko mjue ya kwamba kama zile sheria mnatunga mpya, tunataka President kwanza. Watu waende kukaa huko mbali na tupigie President kura kwanza halafu tuje kwa ministers. Hatutaki mtu achaguliwe huku na hatujui mahali anatoka, tunataka tumpigie kura kama tunajua huyu kama Ghai anatoka huko Coast province, tunajua mahali unatoka na kama barabara inaharibika, yeye ndiye anajua.

Com. Wambua: Tumesikia.

Henry Nyongesa Wanasamba: Ya tatu, MPs lazima tuwapigie kura. Hatutaki mtu anatoka bomani anasema huyu ni Permanent Secretary ama huyu ni MP, tunajua anatoka wapi?

Com. Wambua: Wanachaguliwa tu.

Henry Nyongesa Wanasamba: Hapana sisi tunawapigia kura.

Com. Wambua: Mzee, MPs huwa wanachaguliwa na wewe unatuambia lazima wapigiwe kura

Henry Nyongesa Wanasamba: Wapigiwe kura kwa maoni yangu.

Com. Wambua: Si wanapigiwa kura?

Henry Nyongesa Wanasamba: Tupigie President, tumalize tupigie MP.

Com. Wambua: Halafu?

Henry Nyongesa Wanasamba: MPs tuwapigie, hatutaki mtu achaguliwe bure.

Com. Wambua: Okay, umekataa nominations.

Henry Nyongesa Wanasamba: Ndio.

Com. Wambua: Asante. Kuna jambo lingine?

Henry Nyongesa Wanasamba: Ninalo.

Com. Wambua: Endelea

Henry Nyongesa Wanasamba: Tukimaliza hapo, Permanent Secretaries pia wapigiwe kura

Com. Wambua: Okay. Nani mwingine unataka apigiwe kura?

Henry Nyongesa Wanasamba: Tukimaliza hapo tunakuja kwa PCs.

Com. Wambua: Wapigiwe kura pia?

Henry Nyongesa Wanasamba: Pia wapigiwe kura.

Com. Wambua: Taja sasa wale wote unataka wapigiwe kura.

Henry Nyongesa Wanasamba: Mahali watasimamia kwa maana nimesema kila mtu apigiwe kura.

Com. Wambua: Kila mtu apigiwe kura.

Henry Nyongesa Wanasamba: Kuanzia kwa sub-chief hata mukasa.

Com. Wambua: Hata headmaster apigiwe kura?

Henry Nyongesa Wanasamba: Hata headmaster.

Com. Wambua: Hata mtu wa kanisa apigiwe kura?

Henry Nyongesa Wanasamba: Mtu wa kanisa, watu wa kanisa watampigia kura.

Com. Wambua: Haya, tumesikia hiyo.

Henry Nyongesa Wanasamba: Wacha nimalize hii.

Com. Wambua: Maliza.

Henry Nyongesa Wanasamba: Hata nilisikia kwa radio wakati mwingine, Ghai alisema vizuri. Hata kama chief anaweza kupigiwa kura na wakati huo mimi nilikuwa naona hata chief walikuwa wanahesabu hapa majani wanasema wewe umepita huyu kwa kura fulani.

Com. Wambua: Maliza ya mwisho.

Henry Nyongesa Wanasamba: Ufisadi umekosekana.

Com. Wambua: Wakati umekwisha, tafadhali jiandikishe hapo. Kuja hapa mbele Mzee na utaje jina. Fupisha maneno yale ambayo hayakutajwa. Tuambie mapya.

Richard Simiyu Mwalakha: Kwa majina ni Richard Simiyu Mwalakha.

Com. Wambua: Richard?

Richard Simiyu Mwalakha: Richard Simiyu Mwalakha.

Com. Wambua: Endelea.

Richard Simiyu Mwalakha: Nimeonelea ya kwamba ofisi ya President ama President achaguliwe kwa muda wa miaka mitano na tukimchagua tena, awe na mitano ya mwisho aende kupumzika.

Com. Wambua: Imetajwa hiyo.

Richard Simiyu Mwalakha: Imetajwa?

Com. Wambua: Ndio, 2 terms of 5 years each.

Richard Simiyu Mwalakha: Okay. Local Member of Parliament na kama hatimizi matakwa yetu, awe nullified na kisha arudi nyumbani na tuchague mwingine.

Com. Wambua: Right to recall?

Richard Simiyu Mwalakha: Yes.

Com. Wambua: Hiyo imetajwa.

Richard Simiyu Mwalakha: Already?

Com. Wambua: Ndiyo.

Richard Simiyu Mwalakha: Nitataja moja ambayo hawajataja, iko hapa.

Com. Wambua: Endelea.

Richard Simiyu Mwalakha: Mkasa apewe mshahara.

Com. Wambua: Hiyo imetajwa.

Richard Simiyu Mwalakha: Ai!

Com. Wambua: Mkasa ni village elder?

Richard Simiyu Mwalakha: Yes.

Com. Wambua: Alipwe mshahara. Imetajwa hiyo.

Richard Simiyu Mwalakha: Okay. Lack of employment in the country. Proposal ni kwamba tuwe na one-man one-job.

Com. Wambua: Imetajwa hiyo.

Richard Simiyu Mwalakha: Limetajwa?

Com. Wambua: Not even one man, one woman.

Richard Simiyu Mwalakha: Very good.

Com. Wambua: Endelea.

Richard Simiyu Mwalakha: Pombe ya chang'aa, wamegusia hii mambo ama bado? Wameguza hii mambo ya busaa.

Com. Wambua: Wametaja chang'aa.

Richard Simiyu Mwalakha: Chang'aa ihalalishwe maana inakaa kwa vijiji na watu wanaumizana huko. Afadhali waitengeneze kwa njia nzuri na iuzwe kama Uganda katika ma-bar

Com. Wambua: Hiyo ni mpya.

Richard Simiyu Mwalakha: Hiyo ni mpya kabisa, najua hakuna mtu aliguza hiyo.

Com. Wambua: Okay.

Richard Simiyu Mwalakha: Watu wanunue kwa bar lakini isiwe kwa vijiji.

Com. Wambua: Na ipimwe vile inakuwa.

Richard Simiyu Mwalakha: Ipimwe vile inakuwa. Asante. Nafikiri hayo yanatosha.

Com. Wambua: Thank you very much Bwana Richard Simiyu. Jiandikishe huko tafadhali. Songea hapa Mzee. Richard jiandikishe huko.

Richard Simiyu Mwalakha: Nimefikiri nimemaliza.

Com. Wambua: Tufuatane hapa. Sasa Mzee, taja jina na ufanye kama vile Simiyu amefanya. Kama jambo limetajwa usiharibu wakati, tupatie mapya.

Binea Murunga: My names are Binea Murunga.

Com. Wambua: What is the name?

Binea Murunga: Binea Murunga.

Com. Wambua: Binea Murunga, okay endelea.

Binea Murunga: With respect to nominate Members of Parliament, the new constitution should provide the following: nominees to come from special interest groups, a person who has contested in a general election and subsequently lost should not be nominated. Nominated MPs should not be nominated into cabinet and should not be elected to occupy the post of Speaker or Deputy Speaker. Their nominations should be vetted and confirmed by 65% vote of parliament. The new constitution should establish a truly independent Electoral Commission with adequate powers to recognize, organize and control (?) elections.

Com. Wambua: That one has been said.

Binea Murunga: The parliament to have a mechanism or a house of intelligence committee to have control over Government roles but not the President to declare war without permission of the parliament. We need estimate committee, which is meant to scrutinize Government tax and expenditure proposals before they are incorporated in the budget. This means that the parliament should (?) notice and therefore control over the Government budget process. The constitution reform education should be introduced into school civic education curriculum. That the current provision administration in Kenya is a democratic, oppressive, colonial and... (inaudible).

Com. Wambua: What do you want about it? To be scrapped?

Binea Murunga: Yeah, to be scrapped.

Com. Wambua: That has been said.

Binea Murunga: And be replaced by an elected system.

Com. Wambua: That has been said, too.

Binea Murunga: The new constitution should establishe the office of the ombudsman.

Com. Wambua: Ombudsman's office.

Binea Murunga: In every district to listen to complaints from the wananchi.

Com. Wambua: It can be one body with branches so that it (?)

Binea Murunga: Yes. Natural resources and wealth generated within the district be managed by the local Government authorities within the district to be used in development of the local authorities including among others, financing high education of children within our councils, municipalities and towns and that only 25% of the wealth to be generated to the central Government. That is enough. Thank you very much.

Com. Wambua: Asante sana Bwana Binea. Mzee fuata hapo, taja jina.

Laban Makari: Asante.

Com. Wambua: Tuambie mapya.

Laban Makari: Lakini hapana kuwa kama (?)

Com. Wambua: Nitakuambia. Taja jina na uweke hiyo mic karibu.

Laban Makari: Laban Makari

Com. Wambua: Laban?

Laban Makari: Laban Makari Maratanya.

Com. Wambua: Endelea Mzee.

Laban Makari: Mimi naomba serikali, tuna taabu ya watoto wa chokora. Sisi tuna uchungu.

Com. Wambua: Unataka wapewe elimu ya bure?

Laban Makari: Wawasaidie, hatusemi ya bure, serikali isaidie pesa ikuwe chini. Point ya pili, hata kwa hospitali pesa ni juu, wacha mtu akufe, sisi Wazee tutaenda wapi?

Com. Wambua: Unataka tufanye nini?

Laban Makari: Watusaidie tena bei ikuwe chini.

Com. Wambua: Okay, endelea

Laban Makari: Kama ng'ombe wa watoto wasichana iwe ng'ombe sita. Kama mtoto amesoma, pengine watasema na baba yake mwenyewe (?) lakini ng'ombe ikuwe sita.

Com. Wambua: Hiyo tumeelewa.

Laban Makari: Naomba hiyo, sina mengi.

Com. Wambua: Asante sana. Jiandikishe huko Mzee Laban. Mzee taja majina na utuambie kwa kifupi tu.

Moses Baraza Kimalewa: Mimi naitwa Moses Baraza Kimalewa.

Com. Wambua: Moses Baraza?

Moses Baraza Kimalewa: Moses Baraza Kimalewa. Upande wa mashamba nitasema hivi, shamba ambalo liko surveyed linatakikana baada ya miaka kumi, serikali yenyewe irudishe kwa nafasi yake ile shamba ilikuwa surveyed kwa sababu watu wengi wanaumia wakienda kwa lands wanakuliwa pesa mingi sana.

Com. Wambua: Mimi sielewi hapo Mzee, nataka nikuelewe. Naongea naye tafadhali. Unasema land ikiwa surveyed, baada ya miaka 10 serikali ifanye nini?

Moses Baraza Kimalewa: Irudie kwa hiyo shamba na irudishwe kwa nafasi yake vile ilikuwa. Yaani i-survey again.

Com. Wambua: You are saying after 10 years to re-survey?

Moses Baraza Kimalewa: To re-survey again.

Com. Bishop Njoroge: Why?

Moses Baraza Kimalewa: Kwa sababu ukienda lands wanakula watu wengi pesa na hawafanyi kazi yao na watu wanaumia sana.

Com. Bishop Njoroge: Why would you want it to be surveyed twice?

Moses Baraza Kimalewa: Kama kuna kesi ya shamba ya kwamba fulani aliharibu shamba na ilikuwa surveyed na serikali ndio iko na map ya hilo shamba. Mimi tukigombana na wewe na tuenda kwa lands, yule ana pesa ndio atarudisha nafasi yake lakini wanaweza kata shamba lingine na lirudi kwa yule yuko na pesa na yule hana pesa ataumia. Kwa hivyo iwe jukumu la serikali kwamba after 10 years na wa-resurvey na irudishwe kwa nafasi ya acre 10.

Com. Wambua: After 10 years land be re-surveyed by the Government.

Moses Baraza Kimalewa: Ya pili, education inatakikana iwe equal katika Kenya nzima. Kwa mfano sasa tuna computer na unaweza pata kwa province moja ndio iko na computer kwa sababu iko na stima lakini national examination itakuwa sawa katika Kenya. Kwa hivyo, itaonekana kwamba education si sawa katika Kenya.

Com. Wambua: Standardize education.

Moses Baraza Kimalewa: Sawa sawa. Upande wa watoto wa kike katika familia, mtu ambaye amebahatika amezaa wasichana pekee yake, ndio hao watoto waruhusiwe kupata mali ya wazazi wao kama shamba, sio wale wamezaliwa na vijana warudi waseme pia sisi tunataka mashamba na wanaweza kuoleka na watu wengine.

Com. Wambua: Hiyo imetajwa.

Moses Baraza Kimalewa: Imetajwa? Sawa. Lingine ni kuwa watu wa kawaida wanakimbizwa sana kwa chakula ambacho wanaona kinaweza kuwa halali kwao.

Com. Wambua: Hiyo imetajwa.

Moses Baraza Kimalewa: Imetajwa. Kawaida hiyo tu imetajwa, watu wawe free kwa sababu they are in their country.

Com. Wambua: Hiyo imetajwa na wakasema ni chakula.

Moses Baraza Kimalewa: Ni chakula sio chang'aa.

Com. Wambua: Moses, una lingine?

Moses Baraza Kimalewa: Linaweza kupatikana.

Com. Wambua: Toa lingine moja.

Moses Baraza Kimalewa: Lingine, watu ambao wanaweza kujua uhaki wa mtu katika ukoo kama iko kesi ya shamba ibaki familia ama ukoo ndio unaweza kujua huyu mtoto alizaliwa hapa na ana haki ya kupata kuliko kusema advocate ndiye atafanya hiyo keso na hajui vile huyu mtu alizaliwa. Nilikuja late na nitamalizia hapo

Com. Wambua: Hiyo imetoshia.

Moses Baraza Kimalewa: Kama ni bunge, mimi nilikuwa mwanasiasa na ninasema President anastahili kupewa heshima ya kutosha ili awe na mamlaka ya kutawala nchi. Akipungunza madaraka, atakuwa President asiye na sheria

Com. Wambua: Executive President.

Moses Baraza Kimalewa: Yes, na hiyo haitakuwa (inaudible).

Com. Wambua: Unasema ulikuwa mwana siasa.

Moses Baraza Kimalewa: Nilikuwa mwanasiasa.

Com. Wambua: MP ama councillor?

Moses Baraza Kimalewa: Chairman wa party.

Com. Wambua: Chairman wa party.

Moses Baraza Kimalewa: Nataka President awe na mamlaka ya kutosha ndio atawale nchi

Com. Wambua: Asante sana Moses Baraza, tafadhali jiandikishe hapa kwa maoni yako mazuri. Tuendeleo. Sijui huyu Mzee aliruka namna gani na alikuwa mwisho.

Speaker: Nimebahatika Mzee.

Com. Wambua: Sasa bahati yako uitumie vizuri, nimekupa dakika mbili umalize yale ambayo unataka kusema na yawe ni mapya.

Eliud Wafula: Kutoka Chwele. Jina langu ni Eliud Wafula.

Com. Wambua: Endelea Wafula.

Eliud Wafula: Mimi maoni yangu, ya kwanza naona, picha ya raisi iondolewe kwa pesa.

Com. Wambua: Hiyo ilitajwa asubuhi.

Eliud Wafula: Okay, pili (Interjection).

Com. Wambua: Lakini nataka kuuliza tuweke nini hapo badala yake?

Eliud Wafula: Badala yake, waweke kitu kama crown, the Kenya kama simba, ama ishara yoyote ya kuonyesha kwamba ni pesa za Kenya, lakini picha ya rais iondolewe.

Com. Wambua: Okay, endelea.

Eliud Wafula: Ya pili ilisemwa, ya tatu, tuseme ni ya pili; mimi maoni yangu ninaona muda wa raisi President akishapigiwa kura, na aendele. Sio kuweka ati miaka tano, miaka kumi, hapana. Kama vile Councillor, kama vile Mbunge, huwa anaendelea. Kwa hivyo rais aendele miaka yote. Isipokuwa akishakufa, ama aangushwe kwa kura tu, hiyo aondolewe, lakini kwa kusema ati miaka kumi, hiyo hapana. Maoni yangu inasema hivyo.

Baadayo, mishahara ya polisi ichunguzwe na Bunge.

Tano, wanawake wasiwe sawasawa na wanaume, wanawake wawe chini ya waume zao.

Sita, malipo ya County Council kama ma license, local Government imeweka juu zaidi. Kwa hivyo, ni afadhali serikali iingilie. Na iwapunguzie hiyo mizigo wafanyi biashara. Pesa za license ya County Council ziko juu zaidi. Zinaendelea tena kupanda. Nafikiri ni hayo.

Com. Wambua: Kidogo Mzee nikuulize kabla haujaondoka. Umesema, mwanamke asiwe sawa na mwanaume, mwanamke

awe chini ya mwanaume, na ningelipenda kujua kitu kimoja, nataka kujua ni kama tutawapatia wanawake na wasichana nafasi sawa. Nafasi, sio, sijui kama unanielewa? Tuwapatie nafasi sawa ikiwa ni elimu, na wewe uko na wasichana na wavulana, uwapatie nafasi sawa ya elimu, wapewe. (**Interjection**)

Eliud Wafula: Tuseme (**Interjection**)

Com. Wambua: Ngoja nimalize, ngoja nimalize. Ikiwa ni kazi, employment, wapewe nafasi sawa. Ikiwa msichana amesoma akapata degree, na wale ambao wanatakikana wako na degree, apewe na nafasi hiyo itumike kwa nchi, maanake amesoma. Kwa hivyo ningelipenda kuja kama hii neno lako umesema, wanawake wawe chini ya wanaume. Unasema wapoteze hiyo haki ya kuwa wako na nafasi sawa na wanaume, ama ni kule kwa nyumbani unataka ukishakohoa, bibi anyamaze? Unataka nini, sema sawa sawa.

Eliud Wafula: Hapo, wanawake, sio kusema ati kwa elimu vile anafanya kazi, wapi. Lakini nyumbani kwao, hata kama yeye ni mwanamke D.O, na bwana wake ni Chief, aheshimu bwana wake. Sio kusema mimi D.O ndiye huyu. Hapana.

Com. Wambua: Haya tumeelewa. Jindikishe hapo.

Haya, sasa tumekoma, tumefika mwisho wa kikao hiki.

Com. Lethome: Sasa watu wa Chwele, tumefika mwisho wa kikao chetu. Kila kitu kizuri lazima kifike mwisho wake. Na leo, sasa hivi ndio tumefika mwisho wa kikao chetu kwa siku ya leo. Ningependa kuwashukuru sana kwa maoni yenu ya hali ya juu sana. Na maoni ambayo hatujapata kusikia mahali pengine, tumeanza kusikia hapa leo.

Kwa hivyo tunawashukuru sana, na mjue hiyo kazi ambayo mmefanya, tunawahakikishia, kila neno ambalo mmezungumza, limerekodiwa, na litafika huko, na wakati wa kuandika ripoti na kurudisha kwenu mtaweza kuona kuwa yale yote ambayo mmezungumza, haikuwa tu ni mambo ambayo sio muhimu, ni mambo muhimu sana ambayo mmefanya. Na nyote mjue, kila mmoja aliyeshiriki hapa, ameshiriki katika jambo la kihistoria. Tumengoja miaka thelathini na tisa kupata nafasi kama hii. Hatujui tutangoja miaka mia ngapi tena kupata nafasi kama hii. Kwa hivyo hii ni historia, na wewe umeshiriki katika historia. Kwa hivyo tunawashukuru sana.

Na ikiwa bado una maoni, utakwenda nyumbani ulale, ufikirie jambo lingine, usichelewe, unaweza kuandika hayo maoni, na kupitia kwa District co-ordinator wetu, tunaweza kupata hayo maoni yako. Kwa hivyo kwa kufunga kikao, kuna wenyeji wetu wawili hapa. Kwanza tunamshukuru Madam D.O kwa vile tangu jana alikuwa na sisi, leo alikuwa na sisi tunajua ana shughuli nyingi. Ni kwa sababu anajua umuhimu wa kazi hii. Na mlisikia pia yeye kama Mkenya alitoa maoni yake hapa. Na, tunamshukuru sana, na kama ana jambo lolote la kusema, anaweza kuwaambia. Na District Co-ordinator wetu, na wale wote

ambao wamehusika kuifanya kazi hii yetu iweze kufaulu.

Pastor ambaye anasimamia kanisa hili ijapokuwa sikumuona, sijui kama yuko hapa. Tunamshukuru sana, na wale wote ambao wamehusika katika kututayarishia kikao kama hiki. Tunawashukuru sana, Madam D.O pia uwashukuru wale askari ambao wametupatia ulinzi, kuanzia asubuhi, utawashukuru sana. Nafikiri mimi nitawachia sasa Madam D.O na District Coordinator, mtatufungia, na mwisho kabisa tutapata mtu mmoja atufungie kwa maombi. Na tunatangaza kuwa kesho tutakuwa mahali panaitwa Nabanga, nafikiri. Mabanga pole, mimi nitakuwa Mbukusu ngoja.

District Coordinator: Bw. Commissioner Mabanga maana yake ni damu, tulimwaga damu yetu hapo, tukipigania kuwa Wabukusu wakati watu walitaka kuchukua mashamba yetu.

Sasa, ningependa kusema hivi, kwa nyinyi macommissioners kutoka CKRC, kwa uvumilivu wenu kwa kukaa hapa, nimesema asante sana. Sisi watu wa Bungoma vile mnavyoona, pia tunataka nchi hii ielekee mahali fulani. Na, tunajikuta tukiwa kama wananchi wa Kenya, tumefurahi vile nyinyi mmetembea nchi yote nzima, na mkakuja huku Bungoma kusikiliza maoni yetu.

Najua nyinyi mmepata experience, mmeona watu wengi wakitoa maoni, labda yetu si mazuri vile. Lakini nafikiria, hao ambao wamekuja hapa leo, ni watu ambao wameacha kazi yao waone kwamba lazima wao pia washiriki katika kutengeneza hii Katiba. Nimekuwa nikiwaambia Bw. Macommissioner, kwamba constitution ya America iko miaka mia mbili na zaidi sasa. Na tangu itengenezwe, haitengenezwi kila siku. So, nimeambia hawa, watoto na watoto na watoto wa watoto wao, labda hawataona mambo kama haya. So, mmefanya vizuri na asante sana.

Kwa wale maafisa ambao mlitoka, mmekuja na macommissioner, nimesema asante sana. Kuna Committee members, Constitution Committee Members, CCC Members wa Sirisia, Wycliff uko hapa, Bw. Mwalakha uko hapa. ninasema asante sana, Committee member mwingine mwanamke ameenda, na chairman wa CCC ameenda, lakini kesho atakuwa Mabanga huko ndiko kwake sasa. Hata jana alikuwa na sisi huko Sirisia.

Tuna Richard kutoka Kandunyi Constitutional Committee, lakini ametusaidia sana. Gaitano Opilo the translator wetu, retired educational officer, ametusaidia sana. Kuna mama kutoka Mumias School for the deaf, ambaye alifikiri labda sisi hapa tutakuwa na mtu ambaye hasikii, amwonyeshe vile tunazungumza. Lakini kwa bahati mzuri ama mbaya hatukuwa naye. Lakini hatakuwa na sisi kesho tena.

Na kwa watu wote ambao mmekuja, ningependa sasa nimrudishie Madama D.O, kwa sababu Madam D.O ametusaidia sana, sasa yeye ni special D.O mimi nafikiria. Kwa sababu ako na divisions tatu ambazo anachunga. Hata leo ametoka Nalondo ambako tutakuwa kesho. Ametuacha hapa akaenda kuhakikisha venue iko sawa. So, Madam D.O asante sana, nataka nikukaribishe ufunge huu mkutano, na tukimaliza hivyo, tutapata maombi, sijui nani atatupa maombi? Inaonekana watu wawili

wanajua kuomba, so, mmoja atatuomba. D.O karibu.

Madam D.O: Asante sana Bw. Coordinator wetu, Commissioners wetu, wakaaji wa sehemu hii, na viongozi ambao wamevumilia kutoka asubuhi saa tatu mpaka saa hii. Commissioners wetu, we want to thank you so much kwa huo uvumilivu yenu, najua you have sat on very hard chairs, this is unusual maybe in other areas. Lakini katika hapa Chwele mmevumilia, I know at the end of the day maybe the back will be aching seriously. Lakini because mmetupenda, you want us to be part of the constitution of Kenya. You want the people of Chwele to have an input on that document, which we will be proud of, and we thank you for your commitment, we really thank you for that commitment of sitting down for all those hours.

You know naturally a human being is given some hours, maybe eight hours of a day but this is more for you. We thank you so much for that kind of commitment, your staff, thank you too. We know maybe the treatment we have given you is unlike other areas, but you will forgive us, that is what we could manage to offer you. So, may God bless you greatly, watu wetu shukrani kwa ile kazi mmefanya, and that is why we will say the constitution is ours, because we have all participated. May God bless you all. Mtu wa kuomba tafadhali.

Joseph Kitui Mwalakha: Hebu tuombe;

Bwana Mungu, Jehova muumba wa vitu vyote, ukayae juu Mbinguni, Baba ni wakati mwingine tunataka kushukuru jina lako kupitia kwa mwanao Yesu Kristo. Wewe ndiwe uliumba nchi ya Kenya, na ukatupa utawala. Baba Mtakatifu, Mwana wa Mungu Yesu, kupitia kwa jina lako, tulianza na wewe, tunamaliza na wewe.

Haswa Baba, viongozi wetu ambao wametutembelea ambao ni wageni wetu wa heshima, hawa ni Macommissioners, pamoja na Coordinator wetu wa district, pamoja na D.O wetu, Baba pamoja na wazee hawa, ambao wamekaa kwa muda mrefu, wakingoja, wakiona maneno ya nchi yetu itaendelea aje, kwa wakati ujao. Tunasema ni asante.

Viongozi wetu hawa, wasijichukue ya kwamba, labda ndio kwa ajili ya kusoma, lakini najua ni wewe ndiwe uliwachagua, kutoka Mbinguni, au kutoka mikononi mwako. Baba naweka mikononi mwako, upate kuwabariki, vile wanaendelea kuwa na sisi, hata wakimalizia katika area yetu ya Sirisia kesho huko Mabanga, utazidi kuwabariki.

Popote waendapo kulala sisi hatujui lakini wewe unajua, upate kuwa na kila mmoja. Wazee wetu wanaporudi nyumbani, upate kuwabariki. Asante Mtakatifu, kazi hii, wewe ndiwe ulinibariki nikiwa kiongozi wa hapa, Baba chini ya coordinator yetu, Baba nasema ni asante. Utubariki na tunapoenda tutabariki jina lako. Ni katika jina la Yesu Kristo naomba nikiamini. Amen.

Meeting ended at 5.30 p.m.

